10 JUNI, 2026

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Arobaini na Saba — Tarehe 10 Juni, 2026

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Cecilia D. Paresso) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, karibuni katika Kikao chetu cha Arobaini na Saba, Mkutano wa Tatu.

Katibu.

NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

MWENYEKITI: Maswali, tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, sasa ninamwita Mheshimiwa Esther Edwin Malleko, Mbunge wa Viti Maalum, aweze kuuliza swali lake.

Na. 554

Kuboresha Miundombinu ya Masoko ya Mwika na Makuyuni

MHE. ESTHER E. MALLEKO aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuboresha miundombinu ya Masoko ya Mwika na Makuyuni?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Edwin Malleko, Mbunge wa Viti Maalam, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa Masoko ya Mwika na Makuyuni. Kutokana na umuhimu huo Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Moshi inaendelea na mpango wa kuboresha masoko hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Soko la Makuyuni, halmashauri imeanza kwa kutenga shilingi milioni 50 katika mwaka 2025/2026 ambapo hadi Machi, 2026 shilingi milioni 20 zimetolewa kwa ajili ya kuzibua mifereji ya maji na kusakafia baadhi ya mifereji iliyokuwa imebomoka ili kudhibiti matope kipindi cha mvua. Aidha, halmashauri ikishirikiana na Wizara ya Kilimo itajenga soko la kisasa katika eneo la Makuyuni ambapo hadi sasa halmashauri imekamilisha kuandaa hati pacha ambayo ipo kwenye utaratibu wa kukabidhiwa Wizara ya Kilimo. Zoezi hili litafuatiwa na Wizara ya Kilimo kutangaza zabuni ili kumpata mkandarasi atakayejenga soko hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Soko la Mwika, Halmashauri ya Wilaya ya Moshi katika mwaka wa fedha 2025/2026 imetenga bajeti ya shilingi 16,000,000 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya soko hilo na hadi kufikia Machi, 2026 shilingi 15,000,000 zimetolewa na kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Soko la Mwika lina eneo dogo la kufanyia biashara ambapo inawalazimu wafanyabiashara kufanya shughuli zao katika eneo la barabara kuu kwa kupanga bidhaa zao barabarani. Hivyo, Serikali kupitia halmashauri katika bajeti ya mwaka 2026/2027 imetenga shilingi 70,000,000 kwa ajili ya kununua eneo la ekari moja kwa ujenzi wa miundombinu muhimu katika eneo la Mwika. Hatua hii itapunguza msongamano

uliopo kwenye soko hilo na kuboresha mazingira ya kufanyia biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Esther Edwin Malleko, maswali ya nyongeza.

MHE. ESTHER E. MALLEKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa Serikali imeahidi kwamba itajenga soko jipya kwa eneo la Makuyuni; je, ni lini sasa mchakato wa kumpata mzabuni utakamilika ili soko hilo lianze kujengwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, katika eneo la Mwika kumekuwa na msongamano mkubwa sana na inapelekea wakati mwingine wafanyabiashara kupata ajali kutokana na kwamba wanafanya biashara zao barabarani. Ni lini sasa Serikali itatoa fedha hizo na ziweze kwenda kununua eneo ambalo hawa wananchi wanaweza kupata huduma hiyo kwa usahihi zaidi? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimpongeze sana Mheshimiwa Esther Edwin Malleko, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Kilimanjaro, kwa uchapakazi wake na amekuwa mfuatiliaji sana. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jimbo la Moshi Mjini na Moshi Vijijini kwamba Serikali inatambua sana umuhimu wa masoko haya mawili; Soko la Makuyuni kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunaboresha mazingira ya biashara kwa wananchi na tayari tumeshakubaliana na Wizara ya Kilimo na tumeshaandaa hati pacha ambayo itamilikiwa na halmashauri na Wizara ya Kilimo na tuko hatua za mwisho kukabidhi hati pacha hii ya Wizara

ya Kilimo ili Wizara ya Kilimo iweze kupata mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa Soko la Makuyuni. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tuko hatua nzuri sana ya kuhakikisha kwamba tunajenga soko hilo na kuboresha mazingira ya biashara kwa wananchi wa Makuyuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuhusiana na Soko la Mwika tunatambua kwamba soko lile ni dogo na linapelekea wafanyabiashara kupanga bidhaa zao barabarani jambo ambalo ni hatarishi na ndio maana tumekwishatenga shilingi 70,000,000 katika mwaka wa fedha ujao 2026/2027 tunaoanza Julai hii, ili tuweze kununua eneo lenye ukubwa wa ekari moja na kujenga soko ambalo litaondoa adha ya wafanyabiashara kubanana na kupanga bidhaa barabarani. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Asha Feruz, swali la nyongeza.

MHE. ASHA J. FERUZ: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi, nami ninaomba nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri swali langu la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini sasa Serikali itaboresha miundombinu katika soko la mazao lililoko katika Kata ya Somangila na Pembamnazi katika Wilaya ya Kigamboni?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Asha, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Dar es Salaam kwamba yako masoko likiwemo Soko la Somangila ambalo linahitaji kuboreshwa na tayari Serikali tumeweka mkakati wa muda mfupi, wa muda wa kati na muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kwa kushirikiana na halmashauri kutenga mapato ya ndani kuendelea kuboresha masoko hayo, lakini pili kwa kuandaa miradi ya kimkakati kwa ajili ya kujenga masoko mahususi katika maeneo ambayo tunahitaji

kuboresha masoko hayo. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa Soko la Somangila ni miongoni mwa masoko ambayo tutayapa kipaumbele katika mipango yetu ili tuweze kuliboresha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Edward Olelekaita, swali la nyongeza.

MHE. EDWARD O. KISAU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Soko la Mji wetu wa Kibaya ni la muda mrefu kidogo wafanyabiashara wanahangaika kila wakati na mapato ya halmashauri ni madogo sana. Sasa lini Serikali itatuletea angalau shilingi 1,000,000,000 tu ili tuweze kufumua lile soko letu la Kibaya?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Kibaya ni miongoni mwa miji mikongwe sana katika nchi yetu na katika Jimbo la Kiteto kwa Mheshimiwa Edward Olelekaita na ni mara kadhaa Mheshimiwa Mbunge amefuatilia kuhusiana na uboreshaji wa soko hilo. Mimi nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua umuhimu wa kuboresha Soko la Kibaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI nimwelekeze Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kiteto waandae andiko la kimkakati kutokana na umuhimu wa Soko la Kibaya wawasilishe Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI ili tuweze kufanya taratibu kwa awamu kuona uwezekano wa kuboresha soko hilo. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Fagason Nkingwa, swali la nyongeza.

MHE. FAGASON A. NKINGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo langu la Mbongwe ambalo ni Halmashauri ya Mbongwe haina soko kabisa na kwa sababu hiyo Halmashauri ya Mbongwe iko pale Kasosobe, lakini pale Mbongwe hakuna soko hata la uuzaji wa nyanya na kwa sababu taasisi zote za Serikali ziko pale.

Je, nini mpango wa Serikali kuhakikisha inaenda kujenga soko kubwa pale kwenye Halmashauri ya Mbongwe? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, Serikali ilishatoa maelekezo na ndiYo msimamo wa Serikali kwamba maeneo yote ya halmashauri ambayo ni muhimu kwa huduma za kijamii yakiwemo masoko ni kipaumbele katika mipango ya halmashauri na kwa kuwa Mbunge wa Mbongwe, Mheshimiwa Fagason anasema Halmashauri ya Mbongwe haina soko kabisa, ninaomba nitumie nafasi hii kumsisitiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mbongwe kupitia Baraza lake la Madiwani wakae waainishe eneo kwa ajili ya kujenga soko katika Halmashauri ya Mbongwe, waanze kutenga fedha kwenye mapato ya ndani na ikibidi wawasilishe maombi ili Serikali iweze kuwaunga mkono, lakini dhamira ni kuhakikisha kwamba Halmashauri ya Mbongwe inapata soko zuri ambalo litahudumia wananchi katika eneo hilo. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Alan Mvano, swali la nyongeza.

MHE. ALAN T. MVANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nimesimama hapa kushukuru sana Serikali yetu hii inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwa tuliwasilisha ombi la fedha kwa ajili wa soko na tumepokea fedha na ujenzi unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu ni moja tu, Mheshimiwa Naibu Waziri kama atakuwa tayari kwende pamoja Kakonko aangalie maendeleo ya ujenzi na kuhakikisha kwamba sasa ujenzi unakamilika mapema ili kuwanufaisha wananchi wa Kakonko? Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nimpongeze sana Mheshimiwa Alan Mvano, Mbunge wa Jimbo la Kakonko kwa ufuatiliaji wake wa mara kwa mara na nipokee pongezi ambazo amempa Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na ni hakika kwamba, Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa sana ya kuboresha miundombinu ya masoko katika halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba niko tayari tutapanga ili tuone baada ya kumaliza Bunge letu hili tuweze kufika katika Jimbo la Kakonko, tukague miradi ya maendeleo, lakini pia kuona hatua za ujenzi wa soko hilo. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Charles Njama, swali la nyongeza.

MHE. CHARLES M. NJAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya soko letu la Manundu katika Jimbo la Korogwe Mjini ni mbaya sana na katika kipindi cha mvua zilizopita wafanyabiashara wamepata hasara kubwa kwa sababu ya mafuriko kwa sababu ya miundombinu ambayo imechakaa katika soko lile na kuna hatari kubwa ya kupata hatari ya moto ikitokea basi hasara itakuwa kubwa zaidi.

Je, ni lini Serikali itakuwa tayari kwenda kufanya ukarabati na maboresho ya soko lile ili kuendana na hali ya maendeleo ya Mji wa Korogwe Mjini? Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na nimpongeze Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Korogwe Mjini, lakini nirejee kuwasisitiza Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kote nchini akiwemo Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Korogwe kwamba miundombinu ya masoko kwanza ni sehemu muhimu ya huduma kwa jamii, lakini pili, ni sehemu muhimu ya vyanzo vya mapato na nina hakika halmashauri inakusanya mapato katika soko hilo katika Halmashauri ya Korogwe Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni wajibu wa halmashauri kutenga fedha kupitia mapato ya ndani, kufanya matengenezo kuhakikisha soko lile linahuduma muhimu kama maji, vyoo barabara ya kuingia na kutokea kwa kushirikiana na *TARURA*.

Kwa hiyo, nimwelekeze Mkurugenzi watekeleze ukarabati wa soko hilo mapema iwezekanavyo, lakini na sisi Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI tutafuatilia kuona kwamba soko hilo limekarabatiwa. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Tunaendelea, sasa ninamwita Mheshimiwa Edibily Kazala Kinyoma, Mbunge wa Kasulu Vijijini, aweze kuuliza swali lake.

Na. 555

Ujenzi wa Barabara kwa Kiwango cha Changarawe - Asante Nyerere

MHE. EDIBILY K. KINYOMA aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya kutoka Kata za Asante Nyerere na Kata ya Shunguliba kwa kiwango cha changarawe?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Edibily Kazala Kinyoma, Mbunge wa Jimbo la Kasulu Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali imefanya matengenezo ya kawaida kwenye Barabara ya *Uvinza Junction* - Asante Nyerere kwa kuchonga kilometa 11.46 ambapo pia kiwango cha Changarawe kilometa 2.5 kimewekwa kwa gharama ya shilingi milioni 68.41. Aidha, katika mpango wa bajeti ya mwaka 2026/2027, barabara itafanyiwa matengenezo kwa gharama ya shilingi milioni 16 kwa ajili ya kuweka changarawe kilometa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Asante Nyerere – Mwitiri kwa mwaka wa fedha 2025/2026 imechongwa kilometa mbili na itawekewa changarawe kilometa mbili, matengenezo yote yatagharimu shilingi milioni 32. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali imefanya matengenezo ya kawaida katika Barabara ya Shunguliba – Rungwe Mpya katika Kata ya Shunguliba kwa kuchonga kilometa tisa na itawekwa Changarawe kilometa 3 kwa gharama ya shilingi milioni 81.94

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2026/2027 Serikali itafanya matengenezo ya kawaida kwa kuweka changarawe barabara sita za Kata ya Shunguliba kwa gharama ya shilingi milioni 92.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuzijenga, kuzikarabati na kuzifanyia matengenezo barabara zote za mjini na vijijini kote nchini ikwemo barabara za Wilaya ya Kasulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Edibily Kazala Kinyoma, swali la nyongeza.

MHE. EDIBILY K. KINYOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninakushukuru. Kwanza, nimshukuru Waziri, lakini pia niishukuru Serikali kwa kuniona kwa kuniletea kile kipande cha barabara kwa kujenga kwa kiwango cha changarawe, lakini nilitaka niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kipande cha kutoka Asante Nyerere kwenda Mwitiri mpaka Kanenge na kutoka Mwitiri mpaka Kagege vile vipande havina barabara kabisa na inahitaji kama shilingi 310,000,000 tu kidogo na ni kilometa 10 tu, na wananchi walishaanza kuchonga.

Je, Serikali haioni iko haja ya kuunga jitihada za wananchi kwa kuzichonga vizuri zile barabara na kuziwekea changarawe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Kata ya Shunguliba ile kata haina mtandao kabisa wa barabara wa kuunganisha vijiji vyake vitatu, haina kabisa na wananchi wanakosa huduma, barabara haipitiki mpaka magari ya kuchonga na kuchimba visima yalishindwa kupita. Kwa hiyo, ...

MWENYEKITI: Swali Mheshimiwa.

MHE. EDIBILY K. KINYOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali haioni iko haja ya kuweka mpango wa dharura kuzichonga zile barabara angalau zipitike kutoka Shunguliba kwenda Kazage, Kazage kwenda Malalo? Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na nimpongeze sana Mheshimiwa Edibily Kazala Kinyoma, Mbunge wa Kasulu Vijijini kwa ufuatiliaji wake wa mara kwa mara kuhusiana na miradi ya barabara jimboni kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunafahamu ziko barabara katika

Jimbo la Kasulu Vijijini ambazo zimeharibika kufuatia mvua nyingi zilizonyesha, lakini zipo ambazo hazijakarabatiwa kwa muda mrefu na ndio maana katika jibu langu la msingi tunazo bajeti za kwenda kutengeneza barabara hizi; Barabara ya Asante Nyerere lakini na barabara hii ya maeneo ya Kata ya Shunguliba.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba vipande vya barabara hivyo kilometa 10 ambavyo wananchi kwa nguvu zao wamefungua barabara zile kwanza, nikupongeze Mheshimiwa Mbunge na wananchi kwa kuthubutu kuanza ufungua barabara hizo, lakini nikuhakikishie kwamba Serikali ina utaratibu mzuri, kwanza tunazitambua barabara na kuzisajili kupitia mtandao wa *TARURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitumie nafasi hii nimwelekeze Meneja wa *TARURA* Wilaya ya Kasulu na Mkoa wa Kigoma wapitie barabara hizo ambazo ndio mpya zimefunguliwa na wananchi na kuona kama zinakidhi vigezo vya kusajiliwa kuwa sehemu ya mtandao wa *TARURA* wafanye hivyo ili barabara hizo zitambuliwe rasmi na kuanza kutengewa fedha ili Serikali iweze kupeleka fedha kwa ajili ya matengenezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, kuhusiana na barabara za Kata za Shunguliba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tayari tunaendelea na kutangaza zabuni kwa ajili ya barabara zote zilizoathirika hasa barabara zile muhimu na tutahakikisha barabara za Kata ya Shunguliba zinapewa kipaumbele. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mohamed Utaly, swali la nyongeza.

MHE. MOHAMED M. UTALY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Lindi ipo barabara ambayo inajengwa kupitia Mradi wa *TACTIC,* lakini mkandarasi ameshapewa mkataba, lakini anasuasua mpaka sasa katika suala la ujenzi wa barabara hii na Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa

amekutana na mkandarasi huyu lakini bado anaonekana hatakelezi majukumu yake ipasavyo.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, upo tayari kuambatana nami *sako kwa bato* kwenda kuonana na kuzungumza naye ili aweze kurekebisha mwenendo wake na barabara hii ijengwe kwa manufaa ya wananchi wa Lindi? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Manispaa ya Lindi ni moja ya halmashauri ambazo zina Miradi ya *TACTIC* na ikiwemo ujenzi wa barabara za lami na ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Utaly, Mbunge wa Jimbo la Lindi Mjini kwamba tulishapata mkandarasi na amekuwa *site*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nipokee hoja kwamba, mradi huo hauendi kwa kasi inayotakiwa na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwanza, leo tutawasiliana na Meneja wa *TARURA* wa Mkoa wa Lindi ili watupe taarifa rasmi kwa nini mkandarasi huyo hafanyi kazi kwa kasi inayotakiwa na ikiwa kuna vifungu vya kimkataba ambavyo vimekiukwa tutachukua hatua kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nitumie nafasi hii nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kwamba barabara zetu zote za Mradi wa *TACTIC* zinakamilika na barabara hiyo itakamilika.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jackson Kiswaga, swali la nyongeza.

MHE. JACKSON G. KISWAGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Kwanza ninaishukuru Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tumekuwa na barabara ambayo imekuwa ikisumbua kwa

miaka miwili kutoka Magunga – Wasa na sasa mkataba wake umesainiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali, tunayo barabara ya kutoka Mwimbi – Ulete – Isupilo, hii barabara imeharibika sana kutokana na mvua; je, ni lini sasa Serikali itatupandishia hadhi barabara hii ili iweze kujengwa kwa kiwango cha changarawe na ili iweze kudumu kwa muda mrefu? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimthibitishie Mheshimiwa Kiswaga, Mbunge wa Jimbo la Kalenga na bahati nzuri miezi miwili iliyopita nilifanya ziara katika jimbo lake na ni kweli tuliona baadhi ya barabara ikiwemo barabara aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge, ziliathirika sana na mvua zilizomaliza kunyesha msimu uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumeshatoa maelekezo kwa Mameneja wa *TARURA* wa Wilaya na Mikoa kuainisha barabara zote ambazo ziko maeneo hatarishi zaidi na zinaathirika zaidi na mvua ili tuzibadilishe barabara hizo kwenda kiwango cha changarawe, lakini tujenge mifereji, madaraja na makalvati ya kutosha ili kuhakikisha kwamba barabara hizo zinadumu kwa muda mrefu.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Kiswaga na wananchi wa Jimbo la Kalenga kwamba barabara hiyo tutaipa kipaumbele kuhakikisha kwamba tunaiboresha zaidi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Japhet Hasunga, swali la nyongeza.

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, Barabara ya Chimbuya – Ukwile – Chizumbi – *Msamba One* na Barabara ya Vwawa – Gereza la Vwawa – *Old Vwawa* zimekuwa hazipitiki kwa muda mrefu sana. Ni upi mkakati wa

Serikali wa kuhakikisha kwamba hizi barabara zinatengenezwa kwa wakati? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa Serikali ni kuhakikisha kwamba barabara zote ambazo hazipitiki na barabara muhimu zaidi katika maeneo yetu ambazo zinapitiwa na wananchi wengi kwa shughuli za usafirishaji zinapewa kipaumbele, kwanza kwenye bajeti zetu, lakini pili kwenye matengenezo ya dharura.

Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Hasunga, Mbunge wa Jimbo la Vwawa kwamba barabara ulizozitaja tutazipa kipaumbe, kwanza kwenye 60% ambayo tunatangaza, lakini pia kwenye matengenezo ya dharura tutahakikisha kwamba tunazipa kipaumbele kwa ajili ya kutengeneza barabara hizo ziweze kupitika vizuri. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Edifonsi Kanoni, swali la nyongeza.

MHE. EDIFONSI J. KANONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Kalambo katika Kata ya Mpombwe Kijiji cha Chipwa, kutoka makao makuu ya kata kwenye Kijiji cha Chipwa ambacho kipo mpakani mwa Zambia na Tanzania ni kilometa 6.8 hawajawahi kuwa na barabara toka kupata uhuru, lakini kwenye ilani ya mkoa ipo kwenye bajeti ya kujengewa barabara kwa kiwango cha mawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna maporomoko ya utalii ambayo ni ya historia, ni ya pili Afrika yenye urefu wa meta 335. Nini mpango wa Serikali kujenga barabara hii ambayo wananchi wanapata shida kutoka kijijini kwenda makao makuu, hadi watembee kwa mguu ili kwenda kupata huduma za kimsingi? Mpango wa Serikali kupanga bajeti ili kuweza kuijenga barabara hii kwa kiwango cha changarawe.

Mheshimiwa Waziri ninaomba majibu. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ni kweli kwamba katika Jimbo la Kalambo tunayo Maporomoko ya Kalambo *(Kalambo Falls)* ambayo mimi nilipata bahati ya kuyatembelea, ni maporomoko mazuri sana. Kwa hiyo, ninawashauri Waheshimiwa Wabunge wakipata nafasi na Watanzania kwa ujumla kuyatembelea maporomoko yale mazuri sana na marefu ya pili katika Bara la Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba barabara ile inahitaji matengenezo na ninakubaliana na Mheshimiwa Kanoni, Mbunge wa jimbo hilo. Nitumie nafasi hii kwa sababu barabara ile kwa maelezo ya Mheshimiwa Mbunge bado haijasajiliwa *TARURA*. Kwa hiyo, Meneja wa *TARURA* wa Mkoa wa Rukwa na Wilaya ya Kalambo wafike katika barabara hiyo waifanyie tathmini, na kutokana na umuhimu wake kwa shughuli za kitalii na shughuli za usafiri kwa wananchi, waiingize kwenye utaratibu wa kuisajili kwenye mtandao wa *TARURA* ili tuanze kuitengea bajeti kwa ajili ya matengenezo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Morris Makoi, maswali ya nyongeza.

MHE. MORRIS J. MAKOI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Moshi Vijijini Kata ya Mbokomu, Barabara ya Kiboriloni – Mbokomu – Mti Mrefu ina kilometa 13.94. Serikali imekubali kujenga meta 200 kwa awamu, lakini wananchi wa Mbokomu kwa sasa wamehamasishana wanachanga fedha takribani shilingi milioni 400 kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa barabara hii ya lami.

Je, Serikali iko tayari kuungana nao katika jitihada hizi kuhakikisha kwamba hiyo barabara inajengwa zaidi ya hizo meta 200?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jimbo la Moshi Vijijini na hususan katika eneo hilo la Mbokomu na mimi ninawahakikishia tu kwamba, dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kwamba barabara zinajengwa na zinapitika, na ndiyo maana tumeendelea na taratibu kwamba za kuongeza bajeti katika Halmashauri ya Moshi Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaendelea pia kuhakikisha kwamba, kwa kadri tunavyopata fedha tunapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo ili tuweze kufikia lengo la kuikamilisha kwa kiwango cha lami na changarawe kwa kadri itakavyowezekana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Moses Kaegele, swali la nyongeza.

MHE. MOSES L. KAEGELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Nkasi Kusini na hususan Kata ya Kizumbi na Kata ya Ninde, Kijiji cha Lupata, Lyapinda na Msamba havijaunganishwa na aina yoyote ile ya barabara n ani kweli hadi sasa mkandarasi ameshapatikana, lakini hajasaini mkataba.

Je, ni lini Serikali itatoa fedha ili huyu mkandarasi asaini mkataba na kisha kufungua barabara ya kutoka Lupata – Msamba – Lyapinda ili wananchi waweze kupata usafiri na usafirishaji wa shughuli mbalimbali?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia mara kadhaa kuhusiana na ujenzi na ukarabati wa barabara hizo. Mimi nimhakikishie tu Mheshimiwa mbunge kwamba, Serikali tunafahamu kwamba tunahitaji kupeleka fedha kwa ajili ya ukarabati wa barabara hizo na tunaendelea na hatua za kibajeti, tuko kwenye hatua ya kutangaza zabuni, lakini tuko kweye hatua pia za kupata fedha kwa ajili ya matengenezo ya dharura.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutahakikisha tunazipa kipaumbele barabara hizo ili ziweze kutengenezwa na ziweze kupitika vizuri zaidi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Pascal Lutandula, swali la nyongeza.

MHE. PASCAL L. LUTANDULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Kwa niaba ya wananchi wa Chato Kusini ninaomba kuuliza swali la nyongeza.

Ni lini Serikali itatujengea barabara ya kutoka Iparamasa – Imalamawazo ambayo imekuwa ikisababisha adha kubwa kwa wananchi wa Iparamasa mpaka Imalamawazo na kusababisha ajali kwa siku nyingi? Nini kauli ya Serikali itatujengea hiyo barabara? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Lutandula, Mbunge wa Jimbo la Chato Kusini kwa ufuatiliaji wake. Lakini ninafahamu kwamba Halmashauri ya Chato ni moja ya halmashauri ambazo ziko kwenye mpango wa *TACTIC*, lakini ninafahamu kwamba tuna hatua nzuri za kwenda kutekeleza Miradi ya *TACTIC* katika jimbo hilo, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tunafahamu pia bajeti ya *TARURA* kila mwaka imeendelea kuongezeka kwa ajili ya

kufanya matengenezo lakini pia kufungua barabara katika Jimbo la Chato Kusini na Chato Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutaendelea Mheshimiwa Mbunge kuhakikisha kwamba barabara hizo tunazipa kipaumbele zinatengenezwa na kuhakikisha kwamba zinapitika msimu wote wa mwaka na hususan kuanza kuzijenga kwa kiwango cha changarawe. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na sasa ninamwita Mheshimiwa Clayton Revocatus Chipando, Mbunge wa Kigoma Mjini aulize swali lake. Kwa niaba Mheshimiwa Ester Amos Bulaya.

Na. 556

Ujenzi wa Shule Mpya za Sekondari – Kigoma

MHE. ESTER A. BULAYA K.n.y. MHE. CLAYTON R. CHIPANDO auliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga shule tatu mpya za sekondari Jimbo la Kigoma Mjini ikiwemo ya sayansi, sanaa na michezo na shule ya wasichana?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la mheshimiwa Clayton Revocatus Chipando, Mbunge wa Jimbo la Kigoma Mjini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikijenga shule mpya za sekondari nchini na kuongeza miundombinu katika shule zilizopo ili kuendana na ongezeko la wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2021/2022 – 2025/2026, Serikali imetoa shilingi billioni 5.6 kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya nne za sekondari za Businde Mpya, *Mjimwema Hill*, Kimpampa na Burega, madarasa 152, maabara 24 na kiwanja kimoja cha michezo mbalimbali katika Shule ya Sekondari Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mpango wa Serikali wa ujenzi wa shule za wasichana ilikuwa shule moja kwa kila mkoa ambapo shilingi bilioni 4.35 zilitolewa kwa ajili ya ujenzi wa Shule ya Wasichana Kigoma ambayo ilijengwa katika Halmashauri ya Uvinza, Mkoani wa Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Serikali imetenga shilingi milioni 240 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 10 katika shule tano za sekondari Kigoma Ujiji, Rusimbi, Burega, Bushabani na Businde za Jimbo la Kigoma Mjini. Serikali itaendelea kujenga shule mpya na kuongeza miundombinu katika shule za sekondari nchini ikiwemo katika Jimbo la Kigoma Mjini. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ester Bulaya, maswali ya nyongeza.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, nami niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri ya Mji wa Bunda tuna shule za kimkakati; Shule ya Dkt. Nchimbi, Shule ya Sekondari Sizaki, Sule ya Sekondari Kabasa, pamoja na *Bunda Day* zinachangamoto ya mabwalo, maktaba na mabweni. Zinahitajika zaidi ya shilingi bilioni 1.7 ili kukamilisha mahitaji hayo niliyoyataja kwa ajili ya kuongeza ufaulu kwa watahiniwa, ni lini sasa mtatupatia ili tuweze kukamilisha changamoto hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Serikali imekuwa ikijenga shule za kimkakati za wanawake, za wasichana katika kila mkoa, lakini shule hizi hazina uzio kwa ajili ya kuwalinda mabinti wetu katika shule hizi. Sasa ni lini Serikali, mna mkakati gani wa

kuhakikisha hizi shule zote za wasichana za kimkoa zinakuwa na uzio? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nimpongeze sana Mheshimiwa Ester Bulaya Mbunge wa Jimbo la Bunda Mjini, lakini kwanza ninamthibitishia kwamba, moja ya mpango wa Serikali ni kuhakikisha shule zetu zinakuwa na mabwalo na zile shule za *boarding* zinakuwa na mabweni lakini na maktaba, kwa sababu miundombinu hii ni muhimu sana katika kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba shule zote ulizozitaja tutahakikisha tunaziwekea mpango mkakati wa utekelezaji, lakini hususan shule ambayo inachukua jina la Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, tutaipa kipaumbele cha kwanza cha haraka iwezekanavyo kwa hadhi ya kiongozi wetu ili shule hiyo iweze kupelekewa miundombinu hiyo na nyingine tutaendelea kuzitengea bajeti kwa kadri ya upatikanaji wa fedha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Eric James Shigongo, swali la nyongeza.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili kuhusiana na uzio kwenye shule za kidato cha tano na sita za mikoa za wasichana, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge shule zile 26 zilizojengwa katika mikoa yetu yote 26, kwanza tulianza ujenzi kwa awamu, tulikamilisha majengo yote muhimu kwa gharama ya zaidi ya shilingi bilioni 4.4 kwa shule zote, lakini sasa tutakwenda awamu ya pili kwa ajili ya kuanza ujenzi wa *fence* ili kuweza kuboresha usalama wa wanafunzi katika shule hizo. *(Makofi)*

MHE. ERIC J. SHIGONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Kijiji cha Busikimbi watoto wao wanatembea kilometa 10 kwenda shule na kilometa 10 kurudi nyumbani. Ulikuwepo mpango wa Serikali kwa kujenga shule ya sekondari katika kijiji hicho katika Kisiwa cha Maisome. Ningependa kufahamu, je, Serikali itajenga lini sekondari hiyo?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nimpongeze sana Mheshimiwa Eric Shigongo, Mbunge wa Jimbo la Buchosa, amefuatilia mara kadhaa kuhusiana na shule za msingi lakini pia hata shule za sekondari. Dhamira na mipango ya Serikali ni kuhakikisha wanafunzi wanasoma umbali mfupi iwezekanavyo ili kuepuka wanafunzi kutembea umbali mrefu na wengine kupata changamoto wakati wa kwenda na kurudi shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwa upande wa shule za msingi tunao mpango wa Mradi wa *BOOST* ambao tunaendelea kuainisha maeneo ambayo yana uhitaji wa ujenzi wa shule za msingi na tutahakikisha tunakupa kipaumbele, lakini kwa mpango wa shule za sekondari, tunao mpango wa *SEQUIP*, lakini tunao mpango ambao unakwenda kutekelezwa kwa ajili ya kuchukua wanafunzi wa *double cohort* Januari, 2028.

Kwa hiyo, maeneo yote ambayo yana umbali mkubwa wa wanafunzi tutahakikisha tunayatambua na tayari tumekwishayatambua na tutapeleka fedha kwa ajili ya kujenga shule maeneo hayo ili kupunguza umbali wa wanafunzi katika shule zao. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Cornel Magembe, swali la nyongeza.

MHE. CORNEL L. MAGEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri ya Chato kwa maana ya Jimbo la Chato Kaskazini, ipo shule ya kidato cha sita ya wasichana inaitwa Ilemela Sekondari ambayo shule ile imeanza leo takribani miaka mitano, lakini shule ile iko zaidi ya kilometa 15 kutoka pale kwenda Chato Mjini. Shule ile haina uzio, lakini vilevile haina hata gari la kuweza kuwasaidia watoto wale wanapopata changamoto za kuugua, kuwapeleka hospitali inapotokea.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutuwekea uzio katika shule ile na kutuletea gari kwa ajili ya kuwasaidia watoto wale? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwa bahati nzuri tumekwishaongea mara kadhaa na Mheshimiwa Magembe, Mbunge wa Jimbo la Chato Kaskazini na tulikubaliana kwamba yako maeneo ambayo tuna shule za wasichana, shule mchanganyiko, lakini pia hata shule za wavulana ambao tunahitaji kujenga uzio ili kuboresha usalama wa wanafunzi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatumia nafasi hii kuwakumbusha na kuwasisitiza Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kote nchini kwamba waendelee kutenga fedha kwa awamu kupitia mapato ya ndani ya halmashauri kuanza kujenga uzio au *fence* katika shule zetu ili kuboresha usalama wakati Serikali Kuu inaendelea na mipango kwa ajili ya kuwaunga mkono kuhakikisha kwamba shule zetu zinakuwa na usalama zaidi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Suma Fyandomo, swali la nyongeza.

MHE. SUMA I. FYANDOMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule ya Sekondari Nkunga iliyopo Wilaya ya Rungwe ina wanafunzi 850, ina bweni moja ambalo linabeba wanafunzi 80 tu. Wanafunzi walio wengi wanatembea umbali mrefu. Sasa kwa bweni lile la wanafunzi 80 tumeweka watoto wa kike, watoto wa kiume hawana bweni kabisa.

Sasa je, ni lini Serikali itajenga mabweni kwenye shule hiyo ya sekondari ya Nkunga?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Fyandomo, Mbunge wa Viti Maalumu, lakini nimhakikishie tu kwamba, kwanza Serikali tumeweka sera na miongozo kwamba shule za kidato cha kwanza hadi cha nne ambazo siyo maalumu kwa maana ya kwamba si shule za bweni, basi hatuweki kipaumbele cha hali ya juu cha kujenga mabweni, isipokuwa kama ni mahitaji hatarishi kama maeneo ya wafugaji na maeneo ya aina hiyo.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nikuhakikishie tu kwamba kama shule hiyo ina kidato cha tano na sita tutaipa kipaumbele kwa ajili ya kutafuta fedha kwenda kujenga mabweni katika shule hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa ni shule ya kidato cha kwanza na cha nne, ikiwa halmashauri wanaona umuhimu wa kuwa na mabweni, ninatumia nafasi hii kumsisitiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Rungwe waweke utaratibu wa ndani wa halmashauri kujenga mabweni katika shule hizo ili wanafunzi waweze kupata maeneo mazuri zaidi ya kusoma. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Emanuel Nuwas, swali la nyongeza.

MHE. DKT. EMANUEL Q. NUWAS: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu wananchi wamejenga shule nne za sekondari kutokana na watoto wao kutoka umbali mrefu wa zaidi ya kilometa 12. Tuna Shule ya Mangisa, Dotina, Aloda na Getanyamba.

Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia kumalizia maboma na haya madarasa mawili ili shule hizi ziweze kusajiliwa na kusaidia wanafunzi hawa? *(Makofi)*

MWNEYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa Serikali kwenye uboreshaji wa sekta ya elimu msingi na sekondari ni kuhakikisha kwamba tunakuwa na madarasa ya kutosha kwa ajili ya wanafunzi wetu. Ninaomba nikupongeze Mheshimiwa Dkt. Nuwas, Mbunge wa Jimbo la Mbulu Vijijini, lakini ninawapongeza sana wananchi wa Mbulu Vijijini kwa kuchanga michango yao na kujenga shule hizo nne na kuanza kudahili wanafunzi kwa ajili ya masomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, kupitia fedha za Serikali za mapato ya ndani ya halmashauri, lakini na Serikali Kuu tunayo mipango ya kuhakikisha maboma yote ambayo yamejengwa katika shule zetu yanakamilishwa na kutumika na tutahakikisha katika utekelezaji wa mpango huo tunazipa kipaumbele shule hizo katika Jimbo la Mbulu Vijijini.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Subira Mgalu, swali la nyongeza.

MHE. SUBIRA K. MGALU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwanza kwa kuongoza vikao vizuri, lakini kwa kunipa fursa ya ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Kisutu, Jimbo la Bagamoyo tuna shule moja ya msingi ambayo ilijengwa mwaka 1890, lakini baada ya hatua ya Mheshimiwa Rais kufuta hati ya shamba ya Mchina na kupata ardhi ya kujenga shule, Jumapili iliyopita niliungana na wananchi hao kuanza kujenga shule nyingine ya msingi baada ya ile ya awali kuwa na wanafunzi zaidi ya 1,140 na tulishakamilisha msingi.

Je, Serikali inatupa matumaini gani ya kutuunga mkono kupitia Mradi wa *BOOST* ili kuweza kukamilisha shule hii ya msingi? Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Bagamoyo na amefuatilia mara kadhaa kuhusiana na mahitaji ya ujenzi wa shule mpya ya msingi katika eneo hilo. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba hiyo ndiyo dhamira ya Serikali na ndiyo mipango ya Serikali. Ninawapongeza wananchi wa Jimbo la Bagamoyo lakini pia na menejimenti ya Halmasahuri ya Bagamoyo kwa kuandaa eneo kwa ajili ya ujenzi wa shule nyingine. Ninatoa wito kwamba Mkurugenzi kupitia mapato ya ndani waanze hatua za awali za ujenzi wa madarasa katika shule hiyo mpya na sisi kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, tutaona namna katika bajeti zetu kwenda kuunga mkono kuhakikisha kwamba shule hiyo inajengwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Florent Kyombo, swali la nyongeza.

MHE. FLORENT L. KYOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi. Kwanza, niishukuru Serikali kwa ujenzi wa shule za sekondari ndani ya Jimbo la Missenyi, lakini bado uhitaji ni mkubwa katika Kata za Kyaka na Mutukula.

Je, ni lini sasa Serikali itajenga shule za sekondari katika kata hizo?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango na sera yetu ni kwamba kila kata iwe na shule ya sekondari, lakini kwa zile kata ambazo shule za sekondari zipo, lakini zimekuwa na wanafunzi wengi kupita kiasi, tumekuwa na utaratibu wa kujenga shule nyingine za sekondari ili kuweza kupunguza msongamano katika shule zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Florent Kyombo, Mbunge wa Jimbo la Missenyi kwamba tutazipa kipaumbele Kata ya Mutukula na Kata ya Kyaka katika mipango yetu ya ujenzi wa shule za sekondari ili tuhakikishe huduma ya elimu hiyo inawafikia wanafunzi katika kata hizo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Azza Hamad, swali la nyongeza.

MHE. AZZA H. HAMAD: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Kijiji cha Numbili kilichopo Jimbo la Itwangi wameanzisha ujenzi wa shule ya sekondari kwa kujenga vyumba sita vya madarasa na maboma yameshakwishakamilika.

Je, ni lini Serikali italeta fedha kwa ajili ya kukamilisha majengo haya ili kuwaondolea wanafunzi hawa umbali mrefu wanaotembea kwenda kutafuta elimu ya sekondari? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze sana wananchi wa Jimbo la Itwangi, na Mheshimiwa Mbunge kwa kuchangia nguvu zao na kujenga madarasa sita kwa ajili ya shule hiyo ya sekondari. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali kupitia mapato ya ndani

ya halmashauri na nitumie nafasi hii nimsisitize Mkurugenzi, watenge mapato ya ndani ya halmashauri kwenda kuunga mkono juhudi za wananchi katika ukamilishaji wa miundombinu ya shule hiyo, lakini na sisi Serikali Kuu kupitia Ofisi ya Waziri, TAMISEMI tutaona namna nzuri ya kuhakikisha kwamba shule hiyo inakamilika mapema iwezekanavyo na kuanza kutoa huduma kwa wanafunzi kwa kadri ilivyotarajiwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Abubakari Asenga, swali la nyongeza.

MHE. ABUBAKARI D. ASENGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Kwa kuwa Halmashauri ya Mji wa Ifakara hatujapata mgao wa shule hadi sasa na kwa kuwa Halmashauri ya Mji wa Ifakara ni halmashauri ya pili kwa ukuajia wa uchumi na ongezeko la watu baada ya Manispaa ya Morogoro, na pia kwa kuwa Mkurugenzi wa Halmashauri yangu ameshaandika barua kuomba kusaidiwa kujengewa shule nne kutokana na uhitaji mkubwa wa madarasa; madarasa 20 Kata ya Mwaya, madarasa 18 Kata ya Kibaoni, madarasa 15 Kata ya Ifakara na madarasa 11 Kata ya Viwanja 60.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni nini mpango wa Serikali kutusaidia ujenzi wa shule mpya hizo katika uhitaji mkubwa huo wa madarasa?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Asenga, Mbunge wa Jimbo la Ifakara kwa kazi nzuri kubwa anayoifanya na ninakumbuka jana tu walikuja hapa mezanitukaongea kuhusiana na uhitaji wa shule hizo na mimi nimemuhakikishia kwamba fedha zilizopelekwa kwenye baadhi ya halmashauri kwa ajili ya shule awamu hii ni awamu ya kwanza, lakini zoezi hili ni endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaendelea kupeleka fedha kwa ajili ya kujenga shule, madarasa na miundombinu mingine katika maeneo yote yenye uhitaji, ikiwemo katika Jimbo la Ifakara.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba madarasa uliyoyataja hayo katika shule hizo tutatoa kipaumbele kuhakikisha kwamba tunapeleka fedha na kujenga na kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi wetu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, swali la nyongeza.

MHE. HAWA S. MWAIFUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kuniona. Shule ya Sekondari Itonjanda, imeongezwa madarasa matano pamoja na matundu nane ya vyoo ili kuipanua kuwa *high school* (kidato cha kwanza mpaka kidato cha sita), lakini mpaka sasa shule hii haijasajili wanafunzi wala haijaanza kufanya kazi kwa sababu hakuna *hostel*.

Je, nini kauli ya Serikali juu ya kutokufungua shule hii kwa sababu haina *hostel*, mtuletee *hostel* ili watoto wetu wa Kata ya Itonjanda waweze kupata elimu karibu na maeneo yao? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, Mbunge wa Jimbo la Tabora Mjini, lakini nikuhakikishie tu kwamba safari ni hatua, tumeanza na hatua ya kwanza; kwanza dhamira ya kuipandisha hadhi shule hiyo kuwa kidato cha tano na sita, lakini tumekwenda hatua ya pili ya kujenga madarasa hayo matano na nikuhakikishie kwamba, hatua ya tatu ya kujenga *hostel* na miundombinu mingine ipo kwenye mipango ya Serikali na tutahakikisha tunaikamilisha ili tuweze kudahili wanafunzi wa kidato cha tano na sita kwa ajili ya manufaa ya elimu katika shule hiyo na jimbo hilo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zainab Kawawa, swali la nyongeza.

MHE. ZAINAB R. KAWAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule ya Sekondari ya Anna Magowa iliyopo Wilaya ya Liwale Mkoani Lindi, ni shule ya watoto wa kike, lakini haina ukuta, ni shule ya bweni na ina watoto wa kike. Je, ni lini Serikali, itajenga ukuta kwa ajili ya kusaidia watoto wale wa kike wasome kwa usalama?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli katika shule zetu tunahitaji kuboresha sana usalama na hususani kwa kujenga uzio ili wanafunzi wetu wawe katika mazingira bora na salama zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Zainab Kawawa, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Lindi kwamba hivyo ni miongoni mwa vipaumbele vya Serikali na tutahakikisha kwenye bajeti zetu za mapato ya ndani ya halmashauri, lakini fedha Serikali kuu tunazipa kipaumbele shule kama hiyo ili tuhakikishe tunajenga *fence* na kuboresha usalama kwa wanafunzi wetu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Agnesta Kaiza, swali la nyongeza.

MHE. AGNESTA L. KAIZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule ya Msingi Darajani iliyopo Kimanga, ni shule ambayo haina uzio kabisa, lakini ipo sambamba kabisa na makaburi, kitendo kinachopelekea watoto wetu kushiriki makaburi kuliko jinsi wanavyoshiriki masomo.

Swali langu, ningeomba kufahamu nini mkakati wa Serikali wa dharura wa kujenga uzio kwenye hii shule ili watoto wetu waache kushiriki mazishi na badala yake wajikite katika suala zima la kupata masomo? Ahsante sana.

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nimhakikishie Mheshimiwa Agnesta Lambert, Mbunge wa Jimbo la Segerea kwamba tunatambua changamoto hiyo na kulingana na *location* ya shule lazima tuweke kipaumbele kujenga *fence* ili tuwape utulivu wanafunzi katika masomo.

Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, tumelipokea hilo na tutawasiliana na Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, tuone uwezekano wa bajeti za ndani za dharura ili angalau tuanze hatua za ujenzi wakati Serikali Kuu inajipanga kwa ajili ya kuunga mkono. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaendelea, sasa namwita Mheshimiwa Shaffin Ahmedali Sumar, Mbunge wa Uyui, aweze kuuliza swali lake.

Na. 557

Ujenzi wa Barabara ya Malumba-Mabama-Mwegelezi

MHE. SHAFFIN A. SUMAR aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara kutoka Malumba-*Mabama Centre*- Mwigelezi kwa kiwango cha lami?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Shaffin Ahmedali Sumar, Mbunge wa Jimbo la Uyui kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi na ukarabati wa barabara ili kuboresha usafiri na kuchochea maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa wananchi nchini ikiwemo barabara za halmashauri ya wilaya ya Uyui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini *(TARURA)* ina mpango wa kuijenga Barabara ya Malumba – *Mabama Center* – Mwegelezi yenye urefu wa kilometa 5.37 kwa kiwango cha lami. Katika mwaka wa fedha 2026/2027 Serikali imetenga fedha kiasi cha shilingi milioni 15 kwa ajili ya kufanya usanifu wa barabara hiyo ili kubaini gharama halisi za ujenzi wa barabara hiyo. Aidha, ujenzi wa barabara hiyo unatarajiwa kufanyika katika mwaka wa fedha 2027/2028.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kujenga na kukarabati barabara zote nchini ili kuchochea shughuli za kiuchumi na kijamii ikiwemo barabara za Halmashauri ya Wilaya ya Uyui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Shaffin Sumar, maswali ya nyongeza.

MHE. SHAFFIN A. SUMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza na naishukuru sana Wizara kwa majibu mazuri lakini ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hii barabara ilitokana na ahadi ya Mgombea Mwenza mwaka 2020 ambapo alipokuwa amepita kuomba kura ambaye sasa hivi ni Rais wetu, Dkt. Samia

Suluhu Hassan, kwa kuona mapokezi mazuri kutoka kwa wananchi, aliahidi kwa mapenzi yake kwamba ataijenga hii barabara. Hivi sasa tuna zaidi ya miaka mitano barabara haijawahi kufanyiwa kazi, lakini fedha pia zilizotengwa shilingi milioni 15 kwa ajili ya hii barabara ni chache sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna haja na hoja ya kumaliza hii barabara haraka kwa sababu Mama Samia, anarekodi ya kukamilisha ahadi zake kabla ya wakati. Niiombe sana Wizara, ituongezee bajeti barabara hii ikamilike ndani ya mwaka mmoja kwa sababu ni ahadi ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, tuna barabara ya kutoka Kijiji cha Mabama kuelekea Kijiji cha Ideka, Kijiji cha Tura mpaka Kijiji cha Katunda ambayo kwa miaka mingi haijahudumiwa wala haijakarabatiwa na ina makorongo mengi sana. Nini kauli ya Serikali kuhusiana na utengenezaji wa hii barabara? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mbunge wa Jimbo la Uyui, Mheshimiwa Shaffin Ahmedali Sumar, na amekuwa mfuatiliaji wa mara kwa mara kuhusiana na uboreshaji wa barabara katika Jimbo la Uyui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie tu kwamba kwanza ahadi za viongozi wetu wa kitaifa ni kipaumbele nambari moja kwenye bajeti zetu na ndio maana katika mwaka huu wa fedha tumetenga shilingi milioni 15 kwa ajili ya kufanya usanifu ili kuweza kutambua gharama halisi zinazohitajika kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kilometa 5.37 kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa taratibu za kitaalamu tumejiridhisha kwamba shilingi milioni 15 inatosha kugharamia kazi ya usanifu, lakini baada ya usanifu sasa tutatenga bajeti kwa ajili

ya kuanza ujenzi wa barabara hii kiwango cha lami ili ahadi hiyo iweze kutekelezwa na wananchi wa Jimbo la Uyui waweze kufurahia matunda ya Serikali yao sikivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunafahamu barabara za Mabama na maeneo mengine ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja, ni barabara ambazo zimeathirika na mvua, lakini pia nyingine hazijafanyiwa matengenezo na ndio maana tupo kwenye hatua za mwisho za kutangaza zabuni 60% ya bajeti ya *TARURA* Wilaya na Mikoa kote nchini ili kuhakikisha kwamba barabara hizi zinajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutahakikisha pia barabara hizo Mheshimiwa Mbunge, tunazipa kipaumbele.

MWENYEKITI: Mheshimiwa *Engineer* Amosy Maganga, swali la nyongeza.

MHE. ENG. AMOSY W. MAGANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Misheni ni moja kati ya kata zilizopo katika mji wa Sikonge na baadhi ya barabara zake zipo katika ahadi ya kujengwa kwa kiwango cha lami pamoja na kufungwa kwa taa za barabarani. Je, ni lini sasa Serikali itaanza utekelezaji wa mradi huo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa *Engineer* Maganga, Mbunge wa Jimbo la Sikonge, amefuatilia kuhusiana na ujenzi wa barabara hizi na tumekwishamhakikishia na nirejee kumuhakikishia kwamba tunatambua zipo barabara za ahadi, zipo barabara za kwenye mipango ya kila mwaka ya *TARURA* kuhakikisha kwamba zinajengwa kiwango cha changarawe na kiwango cha lami, lakini pia kuweka taa za barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nikuthibitishie kwamba huo ndio mpango wa Serikali na ndio tamko la Serikali kwamba tutaendelea kutenga fedha kwa awamu kuhakikisha kwamba barabara hizo zinajengwa na wananchi wanapata huduma nzuri za barabara katika Jimbo la Sikonge.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Simon Songe, swali la nyongeza.

MHE. SIMON S. LUSENGEKILE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaishukuru sana Serikali kwa kutujengea majengo mawili; Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na Ofisi ya Mkurugenzi, lakini tunazo changamoto za barabara kutoka barabara kuu Mwagulanja kwenda kwenye Ofisi ya Mkuu wa Wilaya pamoja na Ofisi ya Mkurugenzi ambazo zimekuwa zikiharibika mara kwa mara na zinaendelea kuhudumiwa na *TARURA*.

Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba inazijenga barabara hizi kwa kiwango cha lami ili kufikika kirahisi kwenye Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Songe Lusengekile, Mbunge wa Jimbo la Busega, lakini pia niwapongeze kwa kupata ofisi mpya ya Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi, lakini nimhakikishie tu kwamba barabara zilizokwenda kwenye ofisi hizo kubwa katika wilaya ni kipaumbele cha Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na niitumie nafasi hii nimuelekeze Meneja wa *TARURA* wa Mkoa wa Simiyu na Meneja wa *TARURA* wa Wilaya ya Busega, wafike katika barabara hizo wazifanyie tathmini na kujua kwanza kuziboresha kwa kiwango cha changarawe inagharimu kiasi gani, lakini pili kuboresha kwa kiwango cha lami inahitaji gharama kiasi gani ili Serikali tuweze kufanya maamuzi ya kuanza kuziboresha barabara hizo kwa awamu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Onesmo Merdson, swali la nyongeza.

MHE. ONESMO M. MNKONDYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mbozi Barabara ya Mlowo – Pito - Isansa ni kilometa 13.6 inaenda kwenye Kituo cha Afya Isansa muhimu kabisa, kwanza haipitiki na ipo kwenye ilani ya uchaguzi kujengwa kwa kiwango cha lami. Nini kauli ya Serikali kuhusu barabara hii kwa wananchi wa maeneo hayo ya muhimu sana? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Mnkondya, Mbunge wa Jimbo la Mbozi, lakini nikuhakikishie tu kwamba tunafahamu katika kipaumbele cha Serikali kupeleka barabara, moja ya maeneo ambayo ni kipaumbele cha hali ya juu ni maeneo ya huduma za jamii kama vituo vya afya.

Kwa hiyo, barabara hiyo ambayo inakwenda Kituo cha Afya cha Isansa ni lazima ijengwe iweze kupitika ili wananchi wapate huduma za afya kwa urahisi, tunafahamu kuna wakina mama wajawazito, kuna masuala ya dharura lazima barabara ipitike vizuri ili ikitokea dharura wananchi waweze kupata huduma kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nikuhakikishie tu kwamba msimamo wa Serikali ni kuhakikisha kwamba tunatenga fedha kwa ajili ya kuboresha na kukarabati barabara hizo na kwa sababu tunaendelea na utangazaji wa zabuni kuwapata makandarasi kwa bajeti ya 60%. Nitoe maelekezo kwa Meneja wa *TARURA* wa Wilaya ya Mbozi na Mkoa wa Songwe, waipe kipaumbele barabara hiyo inayokwenda kituo cha afya ili iweze kuboresha huduma za afya kwa wananchi katika maeneo hayo.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, sasa namwita Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, Mbunge wa Chamanzi aweze kuuliza swali lake.

Na. 558

Ujenzi wa Barabara ya Masista – Rufu Nyampombo

MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Barabara ya Masista hadi Rufu Nyampombo ili kuondoa kero kwa wakazi wa Mtaa wa Rufu ambao wanaongezeka kwa kasi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, Mbunge wa Jimbo la Chamazi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa Barabara ya Masista hadi Rufu Nyampombo yenye urefu wa kilometa 1.6 kwa wakazi wa Mtaa wa Rufu, hususani kutokana na ongezeko la makazi katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikiihudumia Barabara ya Masista hadi Rufu kwa kuichonga, kuiwekea changarawe pamoja na kuweka zege katika maeneo korofi. Katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali ilichonga barabara yote, ikaweka changarawe kwa urefu wa meta 820 na kuweka zege meta 168 kwa gharama ya shilingi milioni 104.4. Aidha, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Halmashauri ya Manispaa ya Temeke iliweka zege kwa urefu wa meta 200 kwa gharama ya shilingi milioni 96.68.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali imeweka bajeti ya shilingi milioni 120 kwa ajili ya kuendelea kuboresha barabara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutafuta rasilimali fedha ili kuiwezesha barabara hii kujengwa yote kwa kiwango cha lami.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, swali la nyongeza.

MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa barabara hii imekuwa ikichongwa mara kwa mara na ikifika kipindi cha mvua, barabara hii yote huharibika upya na kupoteza fedha. Je, Serikali haioni ipo haja ya kuijenga barabara hii yote kwa kiwango cha zege ili kuokoa fedha ambazo zimekuwa zikipotea kila mara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, barabara hii ya Rufu Nyampombo ni barabara ambayo inaunganishwa na barabara ya Jimbo la Mkuranga. Je, Serikali haioni ipo haja ya barabara hii ya Rufu Nyampombo na zile za Mkuranga zikajengwa ili kuondoa msongamano uliokuwepo *Kilwa road*?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, Mbunge wa Chamazi na nimhakikishie tu kwamba dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kwamba barabara zetu zote za mijini na vijijini zinapitika msimu wote wa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua kwamba Mheshimiwa Mbunge, amefuatilia mara kadhaa kuhusiana na ujenzi wa barabara hii yote kiwango cha lami na tayari Serikali imeanza kwa awamu tumeshajenga vipande vya changarawe, vipande vya zege na mpango wa Serikali ni kuhakikisha kwamba barabara yote inajengwa kiwango cha lami ama zege kulingana na mazingira yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali inaona umuhimu huo na tutatenga bajeti kwa awamu kuhakikisha barabara hii inajengwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili kuhusiana na barabara ya Rufu Nyampombo ambayo inaunganisha Jimbo la Chamazi na Jimbo la Mkuranga, ni kweli kwamba barabara hii ikijengwa itapunguza sana msongamano wa *Kilwa road*. Moja ya dhamira ya Serikali ni kupunguza msongamano katika majiji hususani katika Jiji la Dar es Salaam.

Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumepokea hoja hii, tutaifanyia kazi kwa kuipa kipaumbele ili angalau tuendelee kupunguza foleni katika barabara zetu katika Jiji la Dar es Salaam.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, Naibu Waziri TAMISEMI, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, sasa ni Wizara ya Viwanda na Biashara, ninamwita Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, Mbunge wa Hai, aulize swali lake.

Na. 559

Kuanzisha Mji Mdogo wa Kibiashara Eneo la *NDC* Machame

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE aliuliza: -

Je, lini eneo la *NDC* njia panda ya Machame litaachwa kwa wafanyabiashara ili waweze kulitumia na kuanzisha mji mdogo wa kibiashara?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara.

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la *NDC* lililopo njia panda ya Machame, Wilayani Hai Mkoani Kilimanjaro ni eneo lenye ukubwa wa ekari 229.13 linalomilikiwa na Shirika la Taifa la Maendeleo *(NDC)*. Serikali imetenga eneo hili maalum kwa ajili ya ujenzi wa kongani ya viwanda ambapo tayari mshauri mwelekezi ameshapatikana kwa ajili ya zoezi la upangaji wa eneo hilo. Kwa sasa Serikali imewakodishia wananchi eneo hilo kwa ajili ya shughuli za kilimo. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, maswali ya nyongeza.

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Serikali kwa majibu mazuri sana, lakini na mpango mzuri sana.

Swali langu la kwanza, kwa kuwa wananchi wa Hai wako tayari na wamejiratibu kushiriki kwenye kuendeleza mji huu, na wako tayari kuwekeza kwenye mji huu, je, Serikali iko tayari sasa kupokea majina ya wananchi wa Wilaya ya Hai ambao wako tayari kujenga mji huo na kuendeleza kwa kujenga miundombinu mbalimbali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa sasa mkandarasi mwelekezi ameshapewa kazi hii, je, Serikali iko tayari sasa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Hai ili mpango huo uweze kuingizwa kwenye mpango wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai na mpango huo uendane na matakwa na mpango kazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Saashisha, amekuwa akifuatilia jambo hili kwa kipindi kirefu sana na sisi ndani ya sekta yetu ya viwanda na biashara, nimhakikishie kwamba dhamira ambayo wananchi wa Hai wanayo, ndiyo dhamira ambayo sisi ndani ya sekta yetu tunayo. Eneo lile ni eneo la kimkakati na sisi tumekubaliana katika Dira hii ya 2050, pamoja

na kufanya biashara na uchuuzi mwingine, lengo letu ni kuhakikisha tunajenga namna ya kuongeza thamani na mojawapo ni kuwa na kongani za viwanda na ndiyo mpango mzuri ambao tunao katika jimbo lake la Hai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, mshauri mwelekezi huyu ana kazi tatu za msingi; la kwanza kuandaa *master plan* kwa ajili ya mpango wa matumizi, lakini la pili usanifu wa miundombinu, na la tatu tathmini ya mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukikamilisha haya yote, ninamhakikishia kwamba tutakaa vizuri na halmashauri ili tukubaliane, kwa sababu kongani yoyote inayojengwa hapo lazima iwe na mchango kwa shughuli za uzalishaji za wananchi katika eneo husika.

Kwa hiyo nimhakikishie itakuwa kipaumbele, na wawekezaji wa ndani sisi tunawapenda na tunawakaribisha sana na kama watakuwa wanatokea katika eneo la Hai, na wenyewe watakuwa *considered* kwa ajili ya kuendeleza eneo hili muhimu ambalo limekaa kwa muda mrefu. Nikuhakikishie tunalipa kipaumbele na kongani itaenda kujengwa hapo katika eneo la Hai. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ibrahim Shayo, swali la nyongeza.

MHE. IBRAHIM M. SHAYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali kidogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Moshi Mjini ni mji ambao ulikuwa na viwanda vingi sana, lakini sasa hivi Moshi Mjini viwanda vyote vimekufa na kusababisha wananchi wale kukosa ajira. Je, nini kauli ya Serikali kuhusu kufufua viwanda hivyo?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa

swali lake na ninakubaliana naye kwamba mojawapo ya maeneo ambayo yalikuwa na viwanda vingi sana ni pamoja na eneo la Moshi Mjini na kwa kuliona hilo, mwaka na nusu uliopita Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan wakati anafanya ziara katika Mkoa wa Tanga, alielekeza Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kushirikiana na Wizara ya Uwekezaji, kufanya tathmini ya viwanda vyote ambavyo vimekufa na kuja na mkakati wa kufufua viwanda hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya sekta yetu ya viwanda na biashara tumeanza kuifanya kazi hiyo. Pale Tanga tayari tuna viwanda viwili vimeshafufuliwa na tumekutana na wawekezaji kwenye viwanda karibu 14. Kazi hii pia nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge itafanyika na Moshi Mjini. Moshi Mjini kulikuwa kuna viwanda vingi, vingi vimekufa; Kiwanda cha *KNCU*, Kiwanda cha *Kibo Match*, Viwanda vya Kahawa, *Kili Wood* na kwa kuonesha dhamira ya Serikali, tumeshaanza kufanyia kazi. Kuna kiwanda pale cha *Timber (mbao),* kuna Kiwanda cha Viuatilifu, kuna Kiwanda cha Kukoboa Kahawa, vyote hivi tumeshaanza kuviwekea mkakati na vimeanza kufufuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tunatekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan na Moshi pia tumeiweka katika mpango wetu wa miaka sita wa kuhamasisha viwanda na kufufua viwanda na tutaenda kuona matokeo hayo kwa kipindi kinachokuja kifupi. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Judith Kapinga, Waziri wa Viwanda na Biashara tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea naomba kuwatambulisha wageni walioko Bungeni asubuhi ya leo.

Tunaanza na wageni waliokaa Jukwaa la Spika ambao ni wageni sita wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kutoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Nasra Awadh Salmin, Mkurugenzi wa Idara ya Ushauri wa Kisheria. *(Makofi)*

Pia yupo Ndugu Saleh Said Mubarak, Mkuu wa Divisheni ya Uchambuzi wa Sheria na Miswada. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Haji Saleh Haji, Afisa Sheria. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Juma Mohamed Juma, Afisa TEHAMA. *(Makofi)*

Pia yupo Ndugu Mohamed Farid Ali, Afisa Mipango. *(Makofi)*

Wapo pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge; yupo mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi ambaye ni mfanyabiashara kutoka Kigamboni, Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wapo wageni watano wa Mheshimiwa David Silinde ambao ni Maafisa Kilimo wa Shamba la Raha kutoka Mkoani Morogoro. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava ambao ni rafiki zake kutoka Mkoani Shinyanga. *(Makofi)*

Wapo wageni 31 wa Mheshimiwa Yagi Maulid Kiaratu ambao ni wanafunzi na walimu kutoka Manispaa ya Singida. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma ambao ni marafiki zake kutoka Kibaha, Mkoani Pwani. *(Makofi)*

Wapo wageni 15 wa Mheshimiwa Asha Juma Feruz ambao ni familia yake kutoka Kigamboni, Jijini Dar es Salaam na wapo pia watoto wake Mheshimiwa Asha. *(Makofi)*

Wapo wageni saba wa Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara ambao ni walimu wa Shule ya Sekondari ya Sirari kutoka Mkoani Mara. *(Makofi)*

Wapo wageni wanne wa Mheshimiwa Kakulu Buchard Kakulu ambao ni Chama cha Maafisa Rasilimali Watu na Utawala. *(Makofi)*

Yupo mgeni mmoja wa Mheshimiwa Baraka Mwamengo ambaye ni Ndugu Bertison Amoni kutoka Kyela, Mkoani Mbeya. *(Makofi)*

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Cornel Lucas Magembe ambao ni viongozi wa Chama cha Walimu kutoka Mkoani Geita. *(Makofi)*

Yupo mgeni mmoja wa Mheshimiwa Joshua Samweli Nassari ambaye ni Diwani kutoka Kata ya Ngarenanyuki, Mkoani Arusha. *(Makofi)*

Pia, yupo mgeni wa Mheshimiwa Festo Richard Sanga ambaye ni rafiki yake kutoka Mkoani Njombe. *(Makofi)*

Wapo pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wapo wanafunzi 126 na walimu 12 kutoka Shule ya Msingi *Nariva Academy* ya Ngarenanyuki, Wilaya ya Arumeru, Mkoani Arusha. *(Makofi)*

Pia, wapo wanafunzi 60 na walimu 10 wa Shule ya Msingi na Sekondari Josephian kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni wote mlioko Bungeni karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa tunaendelea, sasa Wizara ya Fedha, namwita Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, Mbunge wa Bahi, aulize swali lake.

Na. 560

Uzio kwenye Fedha za Mfuko wa Maji

MHE. KENNETH E. NOLLO aliuliza:-

Je, lini Serikali itaweka uzio wa fedha za Mfuko wa Maji ili zisitumike kwenye matumizi mengine ikizingatiwa adha ya maji bado ni kubwa nchini?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ENG. MSHAMU A. MUNDE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu msingi wa swali hili, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Nollo kwa namna anavyowapambania wananchi wake wa Jimbo la Bahi kwa sababu najua anahitaji wananchi hawa waweze kupata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Taifa wa Maji awali umeanzishwa kwa Sheria Namba 12 ya mwaka 2009 ya Huduma za Majisafi na Mazingira. Kwa sasa mfuko unatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Namba 5 ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 4(1) mpaka (5) ya sheria hiyo, imeelekeza matumizi ya fedha zinazowekwa kwenye akaunti ya Mfuko wa Taifa wa Maji kutumika kwa ajili ya shughuli za maji tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme wazi kwamba pesa zinazoingia kwenye mfuko huo zinatumika kwa shughuli za maji kwa mujibu wa kanuni hii ambayo nimeitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme kwa kifupi kwamba sheria hii na kanuni ambayo imetajwa, Mheshimiwa muuliza swali ana wasiwasi kwamba fedha hizi zikikusanywa hazipelekwi kwenye Mfuko wa Maji kama ipasavyo, lakini nimhakikishie kwamba kwa kushirikiana na Kamati ya Kudumu ya Bajeti, Waziri

wa Fedha anakuja na mabadiliko ya sheria ambayo yataenda kuboresha ufanisi wa kanuni hii kwamba sasa pesa zote zinazokusanywa kutoka kwenye vyanzo vya kuleta kwenye mfuko juu zitapelekwa moja kwa moja kwenye mfuko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Keneth Ernest Nollo, swali la nyongeza.

MHE. KENNETH E. NOLLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani umeona Mheshimiwa Naibu Waziri anavyoambaa ambaa, kuna tatizo kwenye jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliweka chanzo mahsusi kwa ajili ya Mfuko wa Maji, na ni shilingi 50 kwa lita ya mafuta ambayo tunanunua na fedha hizi kwanza zimewekewa ukomo…

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kenneth Nollo, tafadhali ongeza sauti na ukikaribie kipaza sauti.

MHE. KENNETH E. NOLLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Maji ulianzishwa na Bunge na kutafuta chanzo ambacho ni shilingi 50 kwa lita ambayo tunanunua. Bahati mbaya kwanza mfuko huu umewekewa *ceiling* (ukomo) wa matumizi, lakini pamoja na hivyo, fedha hizi zimekuwa zikidokolewa na Serikali badala ya kwenda kutatua tatizo la maji na sote tunajua tatizo la maji hapa nchini ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa msingi wa swali langu ni kwamba, ni lini fedha hizi zitaacha kudokolewa, ziende zikafanye kazi kama ambavyo imetarajiwa na kwa lengo la kutatua tatizo kubwa la maji tulilonalo hapa nchini? *(Makofi)*

Swali langu la pili ni kwamba tumekuwa tunapata *NGOs* na wafadhili wanaosaidia miradi ya maji. Bahati mbaya Serikali inatoza fedha tena kwenye miradi hiyo ambayo tunasaidiwa. Sasa nataka niiulize Serikali, ni lini itaondoa sheria hii, kwa sababu

anayekuja kututatulia tatizo unataka tena umtoze kodi? Nakushukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ENG. MSHAMU A. MUNDE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nollo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kama nilivyotangulia kujibu kwenye swali la msingi kwamba kwa kushirikiana na Kamati ya Bajeti, Waziri kesho anakuja na maboresho ya sheria kwenye ile mifuko ambayo itafanya fedha hizo ziende moja kwa moja kwenye mifuko, lakini pia suala la miradi inayotekelezwa na wadau wa maendeleo kwamba inatozwa kodi, niseme wazi kwamba miradi hiyo inapokuwa inabuniwa au inaletwa kwenye halmashauri au kwenye taasisi za Serikali, taasisi hizo zina uwezo wa kuomba msamaha ya kodi kama wanahitaji na si *automatic* kwamba ukianzisha mradi wa maji kwa mfano kwamba utapata msamaha moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi ni kwamba kama kuna mahitaji ya msamaha wa kodi, taasisi husika inabidi iombe kutoka kwenye Mamlaka ya Mapato Tanzania ili kupata msamaha husika, hasa hasa pengine kama kuna ongezeko la thamani *(VAT)* na hii nitoe rai kwenye taasisi zote, Maafisa Masuuli wanapokuwa na miradi ambayo inaletwa na wahisani au wadau wa maendeleo, basi kabla mradi haujaanza kutekelezwa taasisi hizo kama wanahitaji, zijipange kuomba msamaha na bahati nzuri Mamlaka ya Mapato Tanzania ilishatoa mafunzo kwa viongozi wote wa mamlaka hizo, hasa hasa Serikali za Mitaa wanafahamu, lakini pia viongozi, Mameneja wa *RUWASA* ambao wanatekeleza miradi ya maji, walipata mafunzo kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania ya namna ya kuomba msamaha wa kodi hasa Kodi ya Ongezeko la Thamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mamlaka nyingine zote na taasisi za Serikali. Wanapokuwa na miradi, najua Miradi ya *SEQUIP*, Miradi ya *BOOST* ambayo inatekelezwa kwenye Mamlaka za

Serikali za Mitaa, kama wanahitaji kuomba msamaha wa kodi kwa ile miradi ambayo haina makubaliano ya Serikali ya awali ya kwamba miradi hiyo itakuwa ina msamaha, basi wana wajibu wa kuomba msamaha na wanaomba kupitia mfumo ambao wengi wao wameshapata mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Yahya Mhata, swali la nyongeza.

Waheshimiwa Wabunge, tunaomba tupunguze kidogo sauti.

MHE. YAHYA A. MHATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelekezo ya viongozi wetu wakuu, kwa maana ya Rais, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu ni maagizo. Waziri Mkuu, aliagiza ndani ya Bunge lako hili Tukufu mwezi wa tatu kwamba fedha zote za mifuko zipelekwe moja kwa moja kwenye mifuko.

Naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri, agizo hilo la Waziri Mkuu tangu mwezi wa tatu limetekelezwa kwa kiwango gani? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ENG. MSHAMU A. MUNDE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mhata, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli lilitoka agizo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na Wizara ya Fedha iko kwenye utekelezaji wa agizo hilo. Kwa maeneo ambayo miradi inatekelezwa na mfuko huo au mifuko hiyo, watakubaliana na mimi kwamba yapo maeneo ambayo fedha zimeshapelekwa kwa mujibu wa maelekezo ya Waziri Mkuu ambayo yalitolewa hapa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, Waziri wa Mipango na Uwekezaji.

MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongeze tu kwamba Serikali imechukua kwa uzito maoni ya Waheshimiwa Wabunge juu ya mifuko na kesho Mheshimiwa Waziri wa Fedha ataeleza vizuri namna ambavyo Serikali itatekeleza jambo hilo kwa umakini mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge walielewe hilo kwamba suala la mifuko ya maji, sauti hizi Serikali imezisikia na kesho katika Bajeti ya Serikali Mheshimiwa Waziri wa Fedha ataliweka vizuri. Nashukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Profesa tunakushukuru kwa majibu, na Mheshimiwa Naibu Waziri, Munde Mshamu tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Maji, sasa namwita Mheshimiwa Asia Halamga, Mbunge wa Hanang, aweze kuuliza swali lake.

Na. 561

Ujenzi wa Kisima cha Maji Basodesha

MHE. ASIA A. HALAMGA aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga kisima cha maji katika Kata ya Basodesha?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Asia Abdulkarim Halamga, Mbunge wa Jimbo la Hanang, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa Serikali ni kuhakikisha vijiji vyote 1,575 ambavyo havijafikiwa na huduma ya majisafi na salama vinafikiwa na huduma hiyo ifikapo mwaka 2030 ikiwemo Kijiji cha Basodesh kilichopo Kata ya Basodesha Wilaya ya Hanang, Mkoani Manyara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutatua changamoto ya upatikanaji wa huduma ya maji katika kijiji hicho, Serikali imekamilisha uchimbaji wa kisima kirefu chenye uwezo wa kuzalisha maji lita 20,000 kwa saa aidha, usanifu wa miundombinu ya usambazaji maji umekamilika na Serikali inaendelea kutafuta fedha zaidi ya shilingi bilioni 1.3 kwa ajili ya kuanza utekelezaji. Mradi huo unatarajiwa kunufaisha zaidi ya wananchi 5,620 wa Kijiji cha Basodesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, katika hatua za awali za kupunguza changamoto ya maji katika Kijiji cha Basodesha, Serikali katika mwaka wa fedha 2026/2027 itatekeleza mradi wa maji kwa kutumia chanzo cha Ziwa Bassoutu. Mradi huo unatarajiwa kutekelekezwa ndani ya miezi 12 ambapo miongoni mwa maeneo yatakayonufaika ni pamoja na Diling'ang, Endamudayga na baadhi ya sehemu za Vijiji vya Basodesha na Mureru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Asia Halamga, swali la nyongeza.

MHE. ASIA A. HALAMGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan

kwa kazi kubwa ambayo inaifanya kuendelea kutatua changamoto ya maji katika nchi yetu ya Tanzania.

Swali langu la kwanza, Kata hii ya Basodesha toka dunia imeumbwa hawakuwahi kugusa maji ya bombani, naishukuru Serikali kwa kuchimba visima toka mwaka 2021 lakini hadi sasa usambazaji wa maji haujafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kazi hii kubwa ya Serikali iliyofanywa ninaomba kupata *commitment* ya Serikali sasa kazi hii ambayo imefanyika ni lini wananchi watakunywa maji ya bombani kwa kazi iliyobakia ya usambazaji hasa katika maeneo ya Kijiji cha Basodesha chenyewe, Kijiji cha Gidamo na Kijiji cha Gisiali ni lini kazi hii itaenda kuanza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu la pili, je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kuambatana na mimi na kwenda kuangalia maji wanaokunywa wananchi kwa sasa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Asia Halamga, Mbunge bingwa kabisa kutoka pale Hanang na nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayoifanya, lakini pia napenda kusema kwamba suala la usambazaji wa maji kwa aina ya Mbunge Hanang waliye naye na kwa aina ya Mheshimiwa Rais tuliyenaye Tanzania kazi hiyo haitakuwa ngumu kwenda kuitekeleza kwani ndiyo falsafa ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeshachimba visima vitano katika Jimbo hili la Hanang na katika kata hii ambayo Mheshimiwa Mbunge ameisema ambapo tunafahamu vijiji viwili vinatumia maji kutoka Mlima Hanang, lakini vijiji hivi vitatu ndivyo ambavyo bado usambazaji huujafanyika, lakini nimtoe hofu pamoja na uchimbaji wa visima ambavyo vimeshakamilika Kijiji hiki cha Basodesha pamoja na hivi vijiji vitatu tayari tumeshafanya

usanifu na gharama yake ni shilingi bilioni 4.7 ya kufanya usambazaji mzima wa huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Serikali inaendelea kutafuta fedha, tumekuja na mpango wa muda mfupi katika Kijiji cha Basodesha tunaenda kujenga *point source* ambapo tayari tumeshapata mtu wa kwenda kufanya hiyo kazi na taarifa niliyonayo siku ya tarehe 12 Juni, 2026 tunaenda kusaini mkataba kwa ajili ya kuanza kujenga hiyo *point source*.

Sasa kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji napenda nimwelekeze *RM* ama Meneja wa Mkoa wa Manyara huu mkataba badala ya kusainiwa siku ya tarehe 12 Juni, 2026 ambapo Mheshimiwa Mbunge atakuwa Bungeni usogezwe iwe siku ya wikiendi ambapo Mheshimiwa Mbunge lazima ashiriki katika kusaini mkataba na huu mkataba hautakiwi kusainiwa Mjini Hanang, unatakiwa upelekwe katika kijiji ambacho mradi unapelekwa ili wananchi wakashuhudie kazi kubwa inayofanywa na Mheshimiwa Mbunge wao chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe maelekezo kwa ma-*RM* wote nchini, maeneo ambapo miradi mbalimbali inatekelezwa kuweka jiwe la msingi, lakini kuna miradi ambayo ni ya kuzindua kuna kiwango, naelekeza ma-*RM* wahakikishe kwamba wazinduaji wa miradi wawe ambao wanakuja kutafuta fedha kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambao ni Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge watashiriki katika kuzindua ama kuweka jiwe la msingi kulingana na miradi ambayo tutakuwa tumeipanga badala ya kuita watu wengine ambao hata hawajui pesa inapatikana wapi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nasisitiza sana hili kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, Waheshimiwa Wabunge ambao wanakuja Bungeni kupambania hizi fedha akiwemo Mheshimiwa Asia Halamga wawe sehemu ya kuhakikisha kwamba wanashuhudia utiaji wa saini, uzinduzi wa miradi na uwekaji wa jiwe la msingi kuhakikisha

kwamba ile *ownership* na wananchi wao washuhudia kwamba kweli mwakilishi wao anafanya kazi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili mtumishi wa wananchi wa Wana-Hanang amesema mimi ni nani nikatae kuongozana naye kwenda mpaka Hanang, kwenda kuiwakilisha Serikali na kujionea changamoto ya wananchi wa Hanang, niko tayari kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Andrea Mkumbo, Naibu Waziri wa Maji tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi namwita Mheshimiwa Zuberi Yahya Mfaume, Mbunge wa Morogoro Kusini, sasa aulize swali lake; kwa niaba yake Mheshimiwa Abubakari Asenga.

Na. 562

Ujenzi wa Kituo cha Polisi Mtamba

MHE. ABUBAKARI D. ASENGA K.n.y. MHE. ZUBERI Y. MFAUME aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga upya Kituo cha Polisi Mtamba kilichobomoka mwaka 2014 na shughuli zake kufanyika katika ofisi ya kijiji?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu swali la mheshimiwa Zuberi Yahya Mfaume, Mbunge wa Morogoro Kusini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Mtamba, Kata ya Kisemu baada ya kituo cha

awali kubomoka kutokana na uchakavu. Ujenzi wa kituo kipya umefikia kwenye hatua ya umaliziaji ambapo kazi iliyobaki ni kuweka vioo vya madirisha na mifumo ya maji safi na maji taka na fedha kiasi cha shilingi 13,000,000 kinahitajika. Fedha hizo zitatolewa na Ofisi ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro mwezi Julai, 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Abubakari Asenga, swali la nyongeza.

MHE. ABUBAKARI D. ASENGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana Serikali kwa majibu mazuri na Mheshimiwa Mfaume alikuwa na maswali alikuwa na ombi moja na mimi nitakuwa na maswali mawili madogo ya nyongeza;

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi la Mheshimiwa Mfaume ni kwamba wakati...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Asenga uliza maswali ya nyongeza kama unalo moja uliza moja kama...

MHE. ABUBAKARI D. ASENGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza anasema wakati kituo hicho cha polisi kikiendelea kujengwa, je, Serikali haioni umuhimu wa kupeleka magari ya doria katika tarafa hizo tatu kutokana na uhalifu mwingi kuongezeka kutokana na uchimbaji wa madini na uuzaji wa karafuu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, tunaishukuru Serikali hii ya Watanzania chini ya Chama Cha Mapinduzi kwa ujenzi wa kituo kizuri cha polisi cha Wilaya ya Kilombero tangu Uhuru, kituo cha polisi kimekamilika lakini hakijazinduliwa kwa sababu hakuna *furniture*. Je, ni lini Serikali itapeleka pesa kwa ajili ya *furniture* na kituo hicho kianze kufanya kazi? Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na nimpongeze sana Mheshimiwa Asenga kwa niaba ya Mheshimiwa Zuberi kwa maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza lilikuwa ni suala la umuhimu wa kupeleka gari katika kituo hicho au katika kata hizo tatu na hilo ni kutokana na hali ya uhalifu katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili kimsingi ni swali namba 563 katika maswali ya leo, lakini kwa sababu limeulizwa kwenye swali namba 562 kama ni sehemu ya swali (b) au swali la nyongeza kwenye swali la msingi napenda kumjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba tunaona umuhimu wa kupeleka usafiri kwenye eneo hilo na nimwahidi tu kwamba tutawasiliana na Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Morogoro ili kuona magari yale yaliyopo katika wilaya kama hayajatosheleza sana, basi tuone namna ya kuweza kuongeza usafiri kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali la (b) la uzinduzi wa kituo ambacho tayari kimejengwa lakini kimekosa *furniture,* nataka nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba tutahakikisha kwamba kwenye mwaka wa fedha 2026/2027 tunapeleka *furniture* ili kituo hicho kiweze kuzinduliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dotto Bahemu, swali la nyongeza.

MHE. DOTTO J. BAHEMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata ya Kabanga Wilaya ya Ngara kuna wananchi walijenga kituo cha polisi kinaitwa Julilwigwa zaidi ya miaka saba kile kituo hakijaanza kufanya kazi na jengo lilishakamilika. Polisi wanasema kwamba kuna baadhi ya kitu ambavyo havikukamilika katika kile kituo kama sehemu ya kuhifadhia silaha, kuwa na *ceiling board* ya zege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa je, Serikali ipo tayari kumalizia kile kituo ili wananchi waendelee kupata usalama katika eneo hilo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na nikushukuru na nimpongeze sana Mheshimiwa Dotto kwa kuendelea kufuatilia kwa karibu sana hali ya usalama kwenye jimbo lake hasa katika eneo hili la Kata ya Ngara. Niwapongeze sana wananchi kwa jitihada walizozichukua za kuhakikisha kwamba wanashirikiana na Serikali kujenga vituo vya polisi ili kuongeza huduma ya usalama kwenye maeneo ya karibu na wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ombi ambalo amelitoa Mheshimiwa Mbunge napenda tu kumuahidi kwamba tuko tayari kupeleka watu wetu kufanya tathmini ili kusudi tuweze kujua gharama halisi na hatimaye kuweza kushirikiana na wananchi kumalizia kazi iliyobaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ukizingatia Mji wa Tarime unapanuka kwa kasi ambapo maeneo ya pembezoni kama Kata za Kenyamanyori, Kitare, Nyandoto na Nkende yanakuwa na ongezeko kubwa sana la watu, shughuli za biashara, madini na uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina mpango gani wa dharura wa kujenga vituo vya polisi kwenye kata hizi ambazo ni *outpost* ili kuweza kuimarisha usalama, kuzuia uhalifu, lakini zaidi kusongeza huduma za Jeshi la Polisi hasa Dawati ya Jinsia karibu na wananchi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na nimshukuru sana Mheshimiwa Esther Matiko kwa swali lake la msingi na muhimu hasa katika eneo la kata hizi tatu ambazo amezitaja, kwa kweli kuna umuhimu mkubwa wa kuhakikisha kwamba kwenye kata hizo tunajenga vituo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kwamba kila kata katika nchi hii kwa upande wa Tanzania bara basi tunajenga kituo cha polisi ili kuhakikishia zaidi wananchi usalama wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kata hizi ambazo amezitaja Mheshimiwa naomba nimwahidi kwamba tutapeleka watu wetu kufanya ukaguzi kuona kati ya kata hizi tatu ni eneo gani kwa dharura tunaweza tukaanza kuweka kituo cha polisi ili kusudi zihudumie na kata za jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Shadya Omar, swali la nyongeza.

MHE. SHADYA HAJI OMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi hii.

Kwa kuwa Serikali inaendeleza jitihada zake za kukarabati vituo vya polisi ambavyo vilipata kadhia, lakini imekuwa inaonekana inachukua muda sana na mitaa imekuwa bila vituo vya polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina mkakati gani wa kumaliza vituo hivi ili ulinzi na usalama uendelee kupatikana katika mitaa yetu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na nimshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Shadya Haji Omar kwa anavyofuatilia kwa karibu

masuala ya kiulinzi katika maeneo aliyoyataja na hasa kule katika Jimbo la Tumbatu, najua yeye ni mdau kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kwamba jitihada za Serikali za kuhakikisha kwamba tunajenga vituo vya polisi zimewekwa kwenye bajeti yetu ya mwaka 2026/2027 ambapo tumetenga takribani shilingi bilioni 202 kwa lengo la ujenzi, ukarabati wa vituo pamoja na ofisi za Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo nataka niwaombe Waheshimiwa Wabunge; moja, katika randama tuliyowasilisha ya bajeti ya mwaka 2026/2027 tuliainisha kwa kina kila mkoa na eneo gani kwa mwaka wa fedha 2026/2027 tutaweza kujenga vituo vya polisi. Yale maeneo ambayo yako nje ya randama hiyo, basi yatakuwa yapo kwenye mpango wetu wa miaka mitano wa ujenzi na ukarabati wa ofisi na vituo vya polisi katika kipindi hiki cha miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Muhsin Ussi, swali la nyongeza.

MHE. MUHSIN HAJI USSI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Malindi, Wadi ya Mlandege tuna Kituo cha Polisi cha Makadara ambacho kwa muda mrefu sasa kimechakaa na kinahitaji kuboreshwa. Kituo hiki cha Polisi Makadara na kinahitaji kuboreshwa, Kituo hiki cha Polisi Makadara kimekuwa muhimili muhimu sana kwa kuwapatia ulinzi wananchi wa maeneo ya makadara na maeneo jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini Mheshimiwa Waziri ama Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari kuambatana na mimi kukagua miundombinu hiyo ili kwa makusudi Serikali ifanye jitihada ya kufanya ukarabati kituo hicho cha polisi? Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Ussi na kwa kweli Kituo cha Polisi anachokiongelea cha Makadara nakijua na kipo mjini na hali yake haiko vizuri sana. Nataka nimwahidi kwamba Serikali iko tayari wakati wowote lakini niombe tu tutoe fursa ya kumaliza Bunge hili na baada ya hapo tupo tayari kuungana na Mheshimiwa Mbunge ili kwenda kutembelea katika Kituo cha Polisi Makadara.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Paschal Chinyele, swali la nyongeza.

MHE. PASCHAL I. CHINYELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, Kituo cha Polisi cha Chang'ombe katika Jiji la Dodoma ni moja ya vituo bora kabisa na vya kisasa ambavyo vimejengwa hivi karibuni kwa ushirikiano kati ya Serikali na wananchi. Hata hivyo kituo hiki kinazungukwa na makazi ya watu waliosongamana.

Je, ni lini Serikali itajenga uzio katika kituo hiki ili kulinda usalama wa kituo pamoja na mahabusu pamoja na polisi wenyewe?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na nimshukuru sana Mheshimiwa Chinyele Mbunge wa Dodoma Mjini ambaye ameulizia kuhusu ujenzi wa uzio wa Kituo cha Polisi cha Chang'ombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahnsate kwanza nikiri ni kweli Kituo cha Polisi cha Chang'ombe kipo kwenye mzunguko wa makazi na mimi mwenyewe binafsi katika njia zangu zisizo rasmi mara baada ya kuteuliwa tu nafasi hii nikiwa Dodoma nilikitembelea hicho bila wenyewe hata pia kujua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri kwamba upo umuhimu kwa mzunguko ule wa wa makazi uliopo kwenye eneo lile na hasa kwa hali halisi ya usalama ilivyo basi kituo hicho kiweze kujengewa

uzio. Nataka nimwahidi tu kwamba tuko tayari kuangalia hali ya fedha ya mwaka wa fedha 2026/2027 endapo itaruhusu na kwa sababu pia yeye ni Makamu Mwenyekiti wetu wa Kamati ya NUU kwa hiyo, nimwahidi kwamba tutajitahidi iwezekanavyo tuweze kumsaidia katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaendelea, sasa ninamwita Mheshimiwa Suleiman Mohamed Rashid, Mbunge wa Mwera aulize swali lake.

Na. 563

Hitaji la Gari Kituo cha Polisi Mwera

MHE. SULEIMAN MOHAMED RASHID aliuliza: -

Je, lini Serikali itakipatia gari Kituo cha Polisi Mwera ili kiweze kutekeleza majukumu yake kwa urahisi?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Suleiman Mohamed Rashid, Mbunge wa Mwera kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeshakipatia Kituo cha Polisi Mwera kilichopo Wilaya ya Magharibi A Mkoa wa Mjini Magharibi magari mawili mapya namba PT 5672 *Toyota Land Cruiser Pickup* na PT 5954 *Toyota Double Cabin Pickup* ili kutoa huduma za polisi katika eneo la Mwera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Suleiman Mohamed.

MHE. SULEIMAN MOHAMED RASHID: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusu gari hizi, mwaka wa fedha 2024/2025 kituo chetu tulipatiwa gari moja lakini baada ya hapo ilihamishwa na ikaenda Mkoa ili aweze kutumia *RTO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nini kauli yake juu ya gari hizo mbili ambazo mpaka sasa hivi ninazungumza hazijafika ndani ya Kituo hicho cha Mwera?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, gari hizi mbili nilizozitaja ni katika mpango wetu wa Jeshi la Polisi wa kugawa magari nchi nzima kila Wilaya, kila *OCD* na kila *OCCID* anapatiwa gari moja. Na haya ndiyo magari mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na Kituo cha Polisi cha Mwera ndio Makao Makuu ya Wilaya ya Magharibi A. Ninafahamu kwamba shaka au wasiwasi wa Mheshimiwa Mbunge unatokana na kwamba kwa sasa kituo hicho cha polisi kipo katika hatua za mwisho za ujenzi kwa maana ya Kituo cha Daraja B.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo shughuli nyingi za magari hayo zimekuwa zikionekana zinafanyika kupitia Kituo cha Polisi cha Bububu. Kwa hiyo ndio maana Mheshimiwa Mbunge amekuwa na hofu kwamba magari hayo hayapo kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini magari haya ni kwa ajili ya Kituo cha Polisi cha Daraja B kiliopo Mwera. Kwa hiyo, mara baada ya kukamilika ujunzi ule magari yale yatatoka kule Bububu anapoona yana-*park* yatakuja ku-*park* pale Mwera na huduma zitaweza kuendelea kutolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ayoub Mohammed, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, sasa ninamwita Mheshimiwa Kiza Hussein Mayeye, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, aulize swali lake.

Na. 564

Kuanzisha Bodi ya Zao la Chikichi

MHE. KIZA H. MAYEYE aliuliza: -

Je, Serikali haioni haja ya kuanzisha Bodi ya Zao la Chikichi na sheria ya zao hili ili kuratibu uzalishaji wake na mnyororo wa thamani?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo inatekeleza Sheria ya Usalama wa Chakula, Sura ya 249 ambayo ilifanyiwa marekebisho kupitia Sheria ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko *(Cereals and Other Produce Act),* Na. 19 ya Mwaka 2009 na hivyo kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko *(COPRA)* lengo likiwa ni kusimamia na kuratibu shughuli za uzalishaji, uchakataji, uhifadhi, masoko na biashara kwenye tasnia ya mazao ya nafaka na mazao mchanganyiko likiwemo zao la chikichi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu mkubwa wa zao la chikichi katika kukuza uchumi na kuongeza ajira kwa wananchi. Mafuta yanayotokana na zao hili yanachangia takribani 60% ya mafuta ya kula yanayoagizwa kutoka nje ya nchi hali inayoonesha kuwa zao hili lina fursa kubwa ya uzalishaji wa bidhaa mbadala wa bidhaa zinazoagizwa kutoka

nje na hivyo kuokoa matumizi ya fedha za kigeni kuagiza kutoka nje ya nchi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kiza Mayeye, swali la nyongeza.

MHE. KIZA H. MAYEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ninaomba kuuliza maswali ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya Mkoa wa Kigoma, Jimbo la Kigoma Kaskazini ndio linaongoza kwa kilimo cha mawese, lakini wakulima hawa wamekuwa wakitumia zana hafifu za uchakatishaji wa kupata mawese.

Je, Serikali ni lini mtaona umuhimu wa kuwasaidia wakulima wa mawese japo kuwapa mashine ili waweze kuzalisha mawese yenye tija? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kwa historia kilimo cha mchikichi leo Malaysia ni nchi ya pili kwa kuzalisha mafuta duniani, mbegu walitoa katika Jimbo la Kigoma Kaskazini. Serikali mmekuwa mkitumia pesa nyingi sana za kigeni kuagiza mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali mtaona umuhimu wa kuleta sheria ya zao la mchikichi ili kuwahakikishia wawekezaji wa viwanda katika mafuta ya mawese? Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nimpongeze sana dada yangu Kiza Mayeye, Mbunge wa Kigoma Kaskazini kwa maswali ya msingi sana yenye faida kwa wananchi wa jimbo lake, lakini na Wana-Kigoma kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja ambalo nimthibitishie, kwamba moja tunatambua umuhimu wa zao la chikichi na ndio maana ukiangalia hata katika bajeti ambayo mlipitisha hapa ya Wizara ya Kilimo mwaka huu katika mazao manne miongoni mwa zao ambao tumelipa kipaumbele ni zao la chikichi na tunakwenda kuzalisha karibu miche milioni tatu ambayo

itakusudiwa kugaiwa bure kwa wananchi ambayo itasaidia kuongeza tija katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo maelekezo ya Wizara kwa Bodi ni kuhakikisha kwamba wanapeleka mashine hizi ndogo ndogo kwa ajili ya kuchakata mafuta ili waweze kuongeza thamani kwa wananchi. Kwa hiyo, tayari hilo jambo lipo katika mpango na tutalitekeleza katika mwaka unaokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini umuhimu wa zao la chikichi tunafahamu na ninafikiri kama nilivyosema kwamba hatua ya kwanza sasa tunataka tuongeze uzalishaji na hatua ya pili maana yake sasa tutatengeneza sheria ambazo zitasaidia kulifanya zao lile kuwa bora ikiwemo kutengenezea sheria katika hatua inayofuatia. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Asha Motto, swali la nyongeza.

MHE. ASHA S. MOTTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mikoa ya Kusini kwa maana ya Mtwara na Lindi imekuwa ikifanya vizuri sana kwenye kilimo cha ufuta na mbaazi. Je, ni lini Serikali itaunda bodi kwa ajili ya mazao haya ili kuleta tija na thamani kwa wakulima wa mikoa hii ya Kusini? Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na nimpongeze vilevile dada yangu Mheshimiwa Asha Motto kwa kazi nzuri ya kuwatetea watu wa Mtwara na sisi kama Wizara tunatambua kwamba mazao ya ufuta na mbaazi ni miongoni mwa mazao ambayo yamekuwa yakifanya vizuri sana katika kipindi cha kama miaka miwili, mitatu iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwa sasa mazao haya yanahudumiwa na Bodi ya *COPRA* lakini tunaendelea kuangalia tija, maana yake tukiona kama zao linaweza kusimama lenyewe

basi Serikali inaweza kulifikiria na kulitafutia bodi katika miaka inayokuja mbele, lakini kwa sasa mazao haya yapo chini ya Bodi ya *COPRA*. Ahsante.

MWENYEKITI: Tunaendelea, sasa ninamwita Mheshimiwa Alan Thomas Mvano, Mbunge wa Kakonko, aulize swali lake.

Na. 565

Kupeleka Zana za Kilimo – Wilaya ya Kakonko

MHE. ALAN T. MVANO aliuliza: -

Je, lini Serikali itapeleka zana za kilimo katika Wilaya ya Kakonko ili kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao ya kilimo?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo inaendelea kutekeleza mpango wa uanzishaji wa vituo 1,000 vya kutoa huduma ya zana za kilimo kwa wakulima katika ngazi ya kata ifikapo mwaka 2030. Lengo likiwa ni kusogeza na kuwawezesha wakulima kupata huduma za zana za kilimo kwa wakati na gharama nafuu ili kuongeza uzalishaji na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza hilo, Wizara imeanzisha vituo 79 katika halmashauri mbalimbali nchini na utekelezaji unaendelea. Aidha, trekta 340 zimenunuliwa na kusambazwa katika vituo hivyo ili kuwezesha upatikanaji wa huduma za zana za kilimo kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2026/2027 Wizara inaendelea na ununuzi wa zana za kilimo kwa ajili ya kuimarisha na kuanzisha vituo vya kutoa huduma za zana za kilimo kwenye halmashauri mbalimbali ikiwemo Kankoko ili kusogeza huduma na kuhamasisha matumizi ya zana za kilimo nchini.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Alan Mvano, swali la nyongeza.

MHE. ALAN T. MVANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza kabisa niishukuru Serikali kwa majibu mazuri yenye matumaini kwa wananchi wa Kakonko kwamba sasa zana za kisasa za kilimo zinakwenda kupelekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri hayo ninayo mambo mawili; jambo la kwanza; kwa kuwa zaidi ya 80% ya wananchi wa Kakonko ni wakulima na wamekuwa wakitumia jembe la mkono kwa muda mrefu, pamoja na mikakati mikubwa ambayo tukonayo ikiwa ni pamoja na mradi mkubwa wa zao la parachichi ambapo tumetenga zaidi ya ekari 1000, vilevile pamoja na mazao mengine ya kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni upi sasa mpango wa Serikali wa haraka kuhakikisha kwamba katika msimu huu wa kilimo unaoanza zana hizi za kisasa zinapelekwa ili kazi hii iweze kuanza hasa katika mradi huu wa ekari 1000 lakini pamoja na kuwasaidia wananchi wengine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ni kwamba pamoja na miradi hii ya kimkakati nilikuwa ninamuomba Mheshimiwa Waziri kama atakuwa tayari afike sasa Kakonko kipindi hiki kifupi kinachokuja ili kutembelea maeneo haya ya miradi na kuweza kuzungumza na wananchi kwa ajili ya kuona namna ya kuongeza tija katika mazao yetu. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nimpongeze vilevile kaka yangu Alan Mvano, Mbunge wa Kakonko kwa maswali yake ya msingi kwa ajili ya wananchi wake na nimthibitishie tu kwamba katika mpango wa haraka kwa sababu katika mwaka wa fedha 2026/2027 Wizara tunanunua zana za kilimo, kwa hiyo, baada ya kufika katika ule mgao basi Halmashauri ya Kakonko itakuwa sehemu ya wale ambao tutawapa mgao mwanzoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusu kufika katika eneo lake niko tayari mara baada ya Bunge kuahirishwa nilishahidi kufika Mkoa wa Kigoma nitakwenda Jimbo lako Kigoma Mjini, Kigoma Kaskazini na maeneo mengine yote ili kuhakikisha kwamba tunawafikia wananchi, tunazungumza nao na kuwahudumia kama ambavyo ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa David Silinde, Naibu Waziri wa Kilimo tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, sasa ninamwita Mheshimiwa Dkt. Regina Christopher Malima, Mbunge wa Viti Maalum, aweze kuuliza swali lake.

Na. 566

Kuwalinda Wazawa Katika Miradi ya Uvuvi na Vizimba

MHE. DKT. REGINA C. MALIMA aliuliza: -

Je, lini Serikali itatunga sheria ya kuwalinda wazawa katika miradi ya uvuvi na vizimba?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana, ninaomba kujibu swali la namba 566 la Mheshimiwa Dkt. Regina Christopher Malima, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Sheria ya Uvuvi, Sura 279 na Sheria ya Usimamizi na Uendelezaji wa Uvuvi katika Bahari Kuu, Sura 388 inawalinda Watanzania katika utekelezaji wa miradi ya uvuvi na ufugaji wa samaki kwa vizimba ambapo sheria imezuia wageni kufanya baadhi ya shughuli kama vile uvuvi

katika maji ya ndani na biashara ya baadhi ya mazao kama vile kaa na kambakochi hai ili zifanywe na Watanzania pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeweka unafuu wa gharama za leseni na tozo mbalimbali kama vile vibali vya uvuvi wa bahari kuu, biashara ya mazao ya uvuvi na ufugaji wa samaki kwa vizimba kwa Watanzania ikilinganishwa na kiasi kinachotozwa kwa wageni. Lengo la hatua hizi za kisheria ni kuwalinda Watanzania kwa kuweka unafuu wa gharama na mazingira rafiki ya ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi itaendelea kufanya maboresho ya sheria kadri inavyohitajika ili kuhakikisha kuwa Watanzania wanaendelea kulindwa katika utekelezaji wa miradi ya uvuvi na ufugaji samaki kwa vizimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Regina Christopher Malima, swali la nyongeza.

MHE. DKT. REGINA C. MALIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa majibu ya Serikali na namna ambavyo Serikali imejipanga kuwalinda wazawa katika miradi ya uvuvi wa vizimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali mawili ya nyongeza; swali la kwanza, ikiwa sheria hizi zilizopo zinawalinda wazawa, kwa nini katika baadhi ya maeneo ikiwemo Kisiwa cha Ukerewe ambacho kinategemea zaidi ya 95% katika masuala ya uvuvi, wazawa ni wachache katika miradi hii ya uvuvi wa vizimba ilhali wageni ni wengi katika miradi hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, je, Serikali ipo tayari kufanya tathmini ya kila katika Kisiwa cha Ukerewe katika masuala ya uvuvi wa vizimba ili na wao wawe wanufaika wa miradi hii badala ya kuwa watazamaji? Ahsante.

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Dkt, Regina Christopher Malima kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nipende kulieleza Bunge lako kwamba mnyororo wa thamani wa ufugaji wa vizimba ni mrefu ukijumuisha uzalishaji wa vifaranga, uzalishaji wa vyakula vya samaki na kwa hiyo kuwezesha ushiriki wa wananchi kuweza kushiriki katika shughuli hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama kunaonekana kwamba wanapatikana watu wengi wageni ndio wanafanya shughuli hizo, sina uhakika sana na suala hilo kwa sababu ufugaji wa samaki kwa vizimba ni eneo jipya na kwa kiwango kikubwa Serikali ndio imeweka nguvu kidogo ya fedha kuweza kuanzisha ufugaji huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo hamasa hiyo inatakiwa iendelee ili upanuzi wa shughuli hizo uonekane dhahiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tathmini kuhusu hali ya Ukerewe tupo tayari kufanya hivyo, lakini ninadhani ushiriki wa Wanaukerewe katika shuguli hizi utagemeana na upatiakanaji wa mitaji na hapa nihamasishe halmashauri za wilaya nchi nzima zianze kutenga fedha hasa zile za 10% kwa maeneo ambayo ya uvuvi kuelekeza huko badala ya kuwapa pesa wananchi kupika vitumbua na kuuza vitumbua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tupeleke maeneo ambayo hapa ni mapya ili wananchi waanze kunufaika na hapa nipende kutambua baadhi ya halmashauri kwa mfano kama Ilemela na Nyamagana wameanza kufanya hivyo na ushiriki wa wananchi unaongezeka na sisi kwa upande wa Serikali tutaendelea kutoa mikopo isiyokuwa na riba kubwa na muda sio mrefu tutaanza pia kutoa fedha ambazo Mheshimiwa Rais amezitoa na ninadhani na hakika Ukerewe pia watanufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nihamasishe mabenki nayo yaanze kusaidia na baadhi yameanza kusaidia NMB wameanza, CRDB wameanza, Benki ya Ushirika nao wameingia nao pia waweze kuwawezesha wananchi wa maeneo ambayo yanaweza kufanya shughuzi za ufugaji wa vizimba wakiwemo Ukerewe waweze kupata mikopo na kushiriki katika shughuli hizo, ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Tinnar Chenge, swali la nyongeza.

MHE. TINNAR A. CHENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kuniona.

Kwa kuwa sasa hivi kuna upungufu mkubwa sana wa samaki kwenye Ziwa Victoria, je, Serikali haioni umuhimu wa kuja na sheria au mwongozo utakaoruhusu vifaranga vya samaki kuzalishwa kwenye vizimba na baadaye vikarudishwa ziwani ili viendelee kukua na kuzaliana, lakini sambamba na kutenga maeneo maalum ambayo yatakuwa ni kwa ajili ya *breeding* na ambapo hakutaruhusiwa kuwa na uvuvi wa aina yoyote ile?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana Mheshimiwa Chenge kwa swali lako zuri lilo na ushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio mwelekeo ambao tunakuwa nao, kama nilivyosema hili ni eneo jipya na linatusaidia kusema ukweli kuongeza uzalishaji wa samaki kwa sababu uvuvi wa asili samaki wameanza kupungua na kwa kiwango kikubwa ni kutokana na uvuvi usiozingatia sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo itabidi tufanye kazi mchanganyiko, mbinu uchanganyiko, kwanza ufugaji wa samaki wa vizimba si mbadala wa uvuvi wa asili, lazima tuwekeze nguvu kubwa sana kulinda uvuvi wa asili kwa sababu ndiyo chanzo

kikubwa cha mazao ya samaki kuliko huu uvuvi ambao ni mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo Serikali imejipanga kuleta sheria hapa Bungeni ili kuunda chombo Madhubuti/mamlaka ya uvuvi kuweza kusimamia raslimali za uvuvi ili tuongeze rasilimali na tuzilinde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni hilo unalolipendekeza ambalo ni kuanza kufanya kitu kinaitwa *restocking,* kutengeneza vifaranga, halafu na kuvipandikiza, halafu na kutenga maeneo ambayo utavandikiza yawe yamehifadhiwa viweze kukua na kuongeza uzalishaji wa samaki. Ahsante sana Mheshimiwa Chenge. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ahmed Ngwali, swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mdowe Haji Kombo.

MHE. MDOWE HAJI KOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri anayoendelea kutupatia hapa, lakini mimi nina swali moja tu dogo la nyongeza ambalo ninapenda kujua ni mpango gani wa Serikali katika suala zima la kuongeza thamani mazao ya uvuvi ili kuongeza kipato kwa wavuvi wetu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana ni kweli kuna haja ya kuongeza thamani ya mazao ya samaki ikiwa ni pamoja na kuwezesha viwanda vya samaki ambavyo vina..., samahani. Ili kuongeza thamani ya samaki itategemea kuongeza thamani ya...

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba arudie swali lake. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Haji, tafadhali ongeza sauti na Waheshimiwa Wabunge tunaomba utulivu ili muuliza swali na mjibu swali waweze kusikilizana.

MHE. MDOWE HAJI KOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi swali langu ni dogo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeomba kujua mpango wa Serikali katika suala zima la kuongeza thamani ya mazao ya uvuvi ili tuweze kuwasaidia wavuvi wetu kupata kipato zaidi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo tatizo kubwa la upotevu wa mavuno ya samaki baada ya kuvunwa na inafikia asilimia kama 30 ya upotevu *(post-harvest loses)*. Ili kuongeza thamani itabidi kuwa na mifumo na teknolojia za kutunza samaki hao wasipotee na hasa mfumo wa vipozeo na Serikali iko inafanya mazungumzo na baadhi ya makampuni ambayo yana teknolojia za kutunza samaki ama kwa njia ya magari au kwa njia ya *fridge* na vifaa vingine vidogo vidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kwa mfano kwa upande wa dagaa, dagaa wengi hupotea uoza kwa hiyo tuna teknolojia pia ya ukaushaji wa hao samaki ili waweze pia kufika masokoni.

Kwa hiyo, Serikali ina mkakati kwa kushirikiana na sekta binafsi kuhakikisha kwamba wavuvi wanapata vifaa vya teknolojia vya kuhifadhi samaki baada ya kuvuna ili kupunguza kiwango hicho cha upotevu wa samaki kwa 30% ambayo ni kiwango kikubwa sana na kwa maana hiyo, hiyo itasaidia kuongeza thamani ya samaki nakushukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Bashiru Kakurwa, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Afya, sasa namwita Mheshimiwa Abdul-Aziz Mohamed Abood, Mbunge wa Morogoro Mjini aweze kuuliza swali lake. *(Makofi)*

Na. 567

Tozo Kwa Wajawazito Vituo Vya Afya

MHE. ABDUL-AZIZ M. ABOOD aliuliza:-

Je, lini Serikali itaondoa malipo yasiyo rasmi kwa wajawazito ikiwemo gharama za vifaa wanapokwenda kujifungua?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, majibu. *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA AFYA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdul-Aziz Mohamed Abood, Mbunge wa Morogoro Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatekeleza Sera ya Afya ya mwaka 2007 inayoelekeza kutoa huduma za matibabu bure kwa makundi maalum ikiwemo akinamama wajawazito na watoto chini ya umri wa miaka mitano pamoja na wazee wenye umri wa zaidi ya miaka 60 wasio na uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeshatangaza rasmi kuanza utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote Awamu ya Kwanza itakayohusisha makundi ya wananchi ikiwa ni pamoja na watoto, wajawazito, walemavu na wazee wasio na uwezo ambapo kundi hili litagharamiwa na Serikali. Kukamilika kwa hatua hii itawezesha wajawazito na watoto chini ya miaka mitano kupata huduma za afya kwa kugharamiwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe rai kwa Waganga Wakuu wa Mikoa na Wilaya pamoja na Waganga Wafawidhi wa vituo vya kutolea huduma za afya kuhakikisha wanatekeleza maelekezo ya Serikali katika kuhakikisha wajawazito wanapata huduma za afya pasipo kikwazo cha fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Abdul-Aziz Abood, swali la nyongeza.

MHE. ABDUL-AZIZ M. ABOOD: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini hali ilivyo katika Manispaa ya Morogoro siyo hivyo. Wajawazito wanapokwenda kujifungua kwenye vituo vya afya, hospitali ya wilaya au hospitali ya mkoa huwa wanatozwa gharama za ziada za gharama chungumzima ili waweze kutimiziwa haja yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, kuna wagonjwa wanaokwenda usiku katika vituo vya afya na hospitali za wilaya na mkoa saa sita, saa saba ya usiku hapewi huduma anaambiwa akalipie *control number* saa saba ya usiku anaipata wapi *control number* kulipia? Sasa naomba kauli ya Serikali kuhusu maswali yangu hayo. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Abood Mohamed kwa kazi nzuri anayoifanya Mkoani Morogoro, tumemuona mara nyingi akichangia vifaa vya kutolea huduma ya afya kwa wananchi wake na akiunga mkono jitihada za Serikali, tunampongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye maswali yake; kwanza kabisa naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan anagharamia gharama za hawa wanawake. Tunatumia zaidi ya shilingi bilioni saba kununua vifaa vya kujifungua hawa wakina mama ikiwemo dawa za kuzuia kutoka damu nyingi, dawa za kuongeza damu, chanjo na huduma zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, hospitali zote nchini hazitakiwi kuwa-*charge* hawa wanawake huduma hizi kwa sababu tayari Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amekwishakulipia hizo gharama. Kwa hiyo, naomba nitoe rai kwa Mganga Mkuu wa Hospitali ya Morogoro na vituo vya afya vyote

Morogoro wafuate Sera ya Afya ambayo inawataka kutoa huduma bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, isitoshe wote tumeshuhudia Mheshimiwa Waziri Mkuu akitolea maelekezo jambo hili kila wakati kwamba wajawazito wasilipishwe hizo gharama. Kwa hiyo, naomba wasifanyekazi kwa mazoea badala yake watekeleze huduma ya kumuhudumia mama na mtoto kama Sera ya Afya inavyoelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, wagonjwa wanaokwenda usiku wanaambiwa *control number*. Huduma za afya ni masaa 24. Hakuna wakati wowote ambapo huduma inafungwa kwa kusema ni usiku au ni mchana, ndiyo maana tunaingia kwa *shift*.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena Mganga Mkuu wa Hospitali ya Morogoro ambaye anawaambia wagonjwa *control number* usiku na huduma hiyo haipo, ahakikishe anaweka mtalaamu wa mfumo usiku huo ili *control number* iweze kupatikana wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *control number* isiwe kikwazo cha kumfanya mama asipate huduma, kwa sababu Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshaelekeza lazima tuwahudumie hawa akinamama kwa upendo na furaha ili tuhakikishe kwamba tunafikia malengo ya *SDGs* kupunguza vifo vya mama na mtoto kama ambavyo inatarajiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Arif Premji, swali la nyongeza.

MHE. ARIF S. PREMJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na tumefarijika sana kusikia maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusiana na Sera ya Afya kwamba huduma hiyo ni bure kuanzia sekunde moja mpaka miaka mitano kwa mtoto mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto 400 mpaka 500 huwa wanazaliwa na ulemavu unaitwa *Anorectal Malformation,* ni ulemavu ambao mtoto anakuwa hana sehemu ya haja kubwa. Hao vijana wanapozaliwa wanahitaji upasuaji wa haraka na upasuaji huo unaenda kwa *phase* tatu, *phase* ya kwanza tu akizaliwa baada ya masaa 24 anafanyiwa upasuaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *phase* hizo zingine huwa zinatokea baada ya kuvuka miaka mitano. Sasa ile huduma ya kusema kwamba anapata bure nanii kwa miaka mitano baada ya miaka mitano ndiyo huduma inakuwa haipo tena na mzazi anakuwa anahangaika na hilo suala na linawapelekea wazazi wengine…

MWENYEKITI: Mheshimiwa swali.

MHE. ARIF S. PREMJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali nini kauli ya Serikali kuhusiana na watu kama hao au watoto kama hao ili waweze kupata huduma ya bure kuanzia mwanzo mpaka mwisho wa tiba? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Arif swali lako ni muhimu sana, lakini haliendani na swali la msingi. Kwa hiyo, ulilete kama swali la msingi.

Mheshimiwa Agnes Hokororo, swali la nyongeza.

MHE. AGNES E. HOKORORO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini ukweli ni kwamba katika vituo vingi vya kutolea huduma za afya bado wajawazito na watoto wadogo wanapokwenda kupata matibabu wanatozwa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatamani kusikia kauli ya Serikali kwa nchi nzima ili vitendo hivi visiendelee kujitokeza katika maeneo mengi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan analipa shilingi bilioni saba kila mwaka kwa ajili ya akinamama wajawazito na watoto ili wapate huduma hizi bure. Naomba nielekeze kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, nielekeze Waganga Wakuu kama nilivyosema kwenye jibu langu, Waganga Wakuu wote wa Hospitali zote nchi nzima kuanzia ngazi ya Taifa, Kanda, Mkoa, Wilaya, Vituo vya Afya hadi Zahanati ni marufuku kumtoza mama mjamzito na mtoto chini ya miaka mitano gharama za matibabu kwa sababu Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amekwishalipa kwa ajili ya kundi hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi, Naibu Waziri wa Afya tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Catherine Canute Joachim, Mbunge wa Viti Maalum aulize swali lake.

Na. 568

Kuimarisha Mfumo wa Malezi na Ulinzi wa Watoto na Vijana

MHE. DKT. CATHERINE C. JOACHIM aliuliza:

Je, upi mpango wa Serikali wa kuimarisha malezi na ulinzi wa watoto na vijana ili kukabiliana na mmomonyoko wa maadili na mienendo hatarishi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, katika kuimarisha malezi na ulinzi wa watoto na vijana ili kukabiliana na mmomonyoko wa maadili na mienendo hatarishi Serikali inafanya yafuatayo:-

(i) Inatekeleza Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto ya miaka mitano kuanzia mwaka 2021/2022 ili kila mtoto wa umri chini ya miaka nane apate huduma jumuishi za malezi na makuzi.

(ii) Vilevile inaendelea na utekelezaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya kuwekeza katika afya na maendeleo ya vijana balehe wenye umri wa miaka tisa hadi kumi na tisa.

(iii) Vilevile inatekeleza Mpango Kazi wa Pili wa Taifa wa miaka mitano wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto kuanzia mwaka 2024/2025.

(iv) Imezindua mkakati wa kitaifa wa miaka 10 wa kukabiliana na mmomonyoko wa maadili kuanzia mwaka 2026/2027; na mwishio

(v) Imeanzisha Kamati ya Kitaifa ya Ushauri juu ya Usalama wa Mtoto Mtandaoni na tayari imeanza kujadili uwezekano wa kuchuja na kuzuia maudhui yasiyofaa kwa watoto wanapotumia mitandao, pia uwezekano wa kuwa na laini maalum ya simu kwa watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hizi zote ni shirikishi kisekta na kijamii na utekelezaji unaanzia ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa hadi Taifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Catherine Joachim, swali la nyongeza.

MHE. DKT. CATHERINE C. JOACHIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naipongeza Serikali kwa kuweka jitihada

mbalimbali ili kuweka ulinzi kwa watoto na vijana. Pamoja na jitihada hizo nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Serikali imezindua mpango wa miaka kumi wa kukabiliana na mmomonyoko wa maadili; je, nini mkakati wa Serikali wa kuhakikisha kunawekwa mifumo katika ngazi ya Serikali za Mitaa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili litakwenda katika Kamati ya Ushauri wa Usalama wa Watoto Mitandaoni. Je, upi mkakati wa Serikali wa kuwajengea uwezo wazazi pamoja na walezi ili waweze kujua jinsi gani watawalea watoto wao katika masuala mazima ya teknolojia? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Catherine Canute Joachim.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na swali la nyongeza la kwanza mkakati gani kuhusu utekelezaji wa mpango wa Taifa wa kudhibiti mmomonyoko wa maadili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati umeanzia kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa ambapo mkakati huu utakwenda sambamba na kuunda Kamati za Maadili kuanzia kijijini, kata, halmsahauri na mkoa na hadi ngazi ya Taifa. Kote huko Wajumbe wa Kamati hizi watakuwa ni shirikishi wakiwemo viongozi wa dini, viongozi maarufu wa kijamii, wawakilishi wa wananchi kwenye maeneo husika, sekta binafsi itakuwepo, mashirika yasiyo ya kiserikali na asasi za kiraia kifupi *clusters* zote za makundi ya kijamii yatakuwa yamewakilishwa pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo sasa hizo taarifa zitokanazo na Kamati hizi zinakwenda kuunganishwa na Mabaraza ya Maendeleo ya Kata hadi kwenda kwenye Halmashauri kwenye vikao vyake vyote hadi *DCC* pale kwa Mkuu

wa Wilaya ambaye ndiyo atakuwa Mwenyekiti kila Wilaya hadi mkoani. Kwa hiyo, huku Taifa kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI tutakuwa tunapokea majumuisho yote na mapendekezo yote ili tuweze kufanyakazi moja ya ku-*edit* au kuboresha ile mipango kitaifa pamoja na sera na sheria zinazohusu eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la ulinzi wa watoto wanapotumia mitandao ya kijamii, wazazi na walezi wameshirikishwa vipi? Tayari tumeshaanza utekelezaji wa mikakati mbalimbali ikiwemo tumetoa mafunzo kwa wawezeshaji *(trainer of trainee)* zaidi ya mia tano, ambao hawa tayari wameishaanza kufundisha walimu mashuleni pamoja na wanafunzi na vikundi vingine vya kijamii kuhusu kuhakikisha watoto wanaelezwa juu ya kutumia mitandao kwa usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi karibia wanafunzi milioni 1.8 hivi wameshapata hayo mafunzo na programu inaendelea na tunatarajia kwamba hawa *trainer of trainees* zaidi ya 500 ambao wametokea pia kila wilaya watashusha chini mpaka kwenye kata kadri ya upatikanaji wa rasirimali za kwetu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Fatma Rembo, swali la nyongeza.

MHE. FATMA A. REMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapomwezesha mtoto wa kike tusimsahau pia mtoto wa kiume ambaye pia anakutana na changamoto nyingi za malezi. *(Makofi)*

Je, Serikali ina mpango gani maalum au mkakati gani maalum wa kuhakikisha kijana wa kiume anajengwa na kulinda ili aweze kuja kuwa kiongozi bora na baba bora wa kesho? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na

nampongeza sana Mheshimiwa Fatma kwa swali lake la nyongeza zuri ambalo linapenda kujua ushiriki wa watoto wa kiume kwenye masuala haya ya malezi na makuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kwamba watoto wote ambao wanasimamiwa chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maluum ni wa jinsia zote na katika mikakati yote tunapotamka neno mtoto, mtoto wa kiume anakuwa ni sehemu. Mfano tunatekeleza mkakati wa vikundi vya malezi vya wazazi, wazazi hawa wanafundishwa jinsi ya kwenda kufanya malezi na makuzi ya watoto, ndani mle wanaume wapo ambao ni baba zao na hawa watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatekeleza elimu kwa jamii inayohusu masuala yanasema Familia Bora Taifa Imara. Tayari wazazi ambao wameshiriki kwenye hii programu au hii kampeni ni kama 550,000 na nusu hivi lakini kati yao laki moja hamsini na saba na pointi ni wanaume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunawafikia watoto hawa kupitia wazazi wao wa kike na kiume, lakini tukienda mashuleni tuna madawati ya ulinzi wa watoto, madawati ya ulinzi wa watoto ni watoto wote wa kike na kiume, na kwenye uongozi pale kiongozi ni mwanamke na mwanaume kwa pamoja. Kuna mabaraza ya watoto tunayafanya. Haya mabaraza ya watoto yanaanzia kijijini, kwenye mitaa, kwenye kata. Haya nayo ni watoto wote wako mle ndani. Tumekuwa na watoto wa kutosha wa kiume wanakwenda kuwakilisha nje ya nchi wakitokea kwenye haya mabaraza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiiangalia sheria ya mtoto ilivyojengwa, inamshughulikia mtoto wa kike na wa kiume. Kwa hiyo, ninapenda tu kusema kwa ufupi tunazingatia masuala haya na ili kuongeza nguvu zaidi tumesajili vyama vya wanaume mbalimbali na siku hiyo nilipowasilisha bajeti tarehe 01 Juni walikuwepo. Lengo ni kuuchukua mtandao wa wanaume uingie, ushike nafasi yake katika kuangalia maslahi ya wanaume, siyo wakubwa tu bali na watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hapa Mheshimiwa Baba Levo tunatarajia kumteua awe Balozi wa Wanaume, lengo ni kwamba kupitia uwezo wake wa kuzungumza nao na kushirikiana nao watuletee zile hoja, wapi tuna-*miss point* katika kusuka mikakati yetu. Hili linakwenda sambamba na Mheshimiwa Kampala pia. Hawa tumewaona wanaweza wakatusaidia sana kwenda vizuri kwenye hii Wizara, ili hili suala mwishowe lipate majibu ya kutosha na ya kina yanayowaridhisha Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jamila Juma, swali la nyongeza.

MHE. JAMILA MAHMOUD JUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, na mimi nichukue fursa hii kuipongeza Wizara ya Jinsia kwa kazi kubwa ambayo inaifanya na ninapenda kuchangia kwamba, tunajua kwamba

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuuliza swali langu, ninajua kwamba Serikali imekuwa ikifanya kazi kwa karibu sana na asasi za kiraia hasa zile ambazo zinajishughulisha na masuala ya ulinzi wa mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu linaelekea, je, Serikali ina mikakati gani sasa ya kushirikiana moja kwa moja na zile asasi au *NGOs* ambazo zinafanya kazi katika masuala ya ulinzi wa mtoto, lakini pia masuala ya elimu na ukuaji wa mtoto? Ninajua kwamba ziko hizi asasi ambazo zinajikita moja kwa moja na haya masuala. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kunipa fursa ya kujibu swali zuri la Mheshimiwa Jamila analotaka kufahamu ushirikiano wetu kati ya asasi za kiraia kwenye masuala ya ulinzi wa mtoto pamoja na elimu kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kusema kwamba ushirikiano unaanza kwa mujibu wa Sheria ya Msajili wa Mashirika

Yasiyo ya Kiserikali na uendeshaji wake ambapo ngazi ya kitaifa tunalo Baraza la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ambalo lilipoingia kwenye kipindi hiki cha utekelezaji wa Serikali ya Awamu ya Sita tuliwataka waupitie upya mwongozo wao wa ushirikiano ya hili baraza lote na Serikali. Wameuhuisha na mara baada ya Bunge hili tutauzindua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba Kamati za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuanzia ngazi kule yanakotekeleza zinakuwa sehemu ya vikao vyote vya Serikali kuanzia ngazi ya kata, wanaingia pale kama wawakilishi wa *NaCoNGO*, wanaleta mipango na mikakato yao na taarifa zao zote na kwenye ngazi ya halmashauri, Mkuu wa Wilaya ndiyo mwenyekiti, anamwakilisha Mheshimiwa Rais eneo hilo. Kwenye ngazi ya mkoa ni Mkuu wa Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwenye *RCC*, kwenye *DCC*, kwenye *Ward DC* kule kwenye kata, hawa watakuwa wanakwenda baada ya kuzindua huu mwongozo mapema Julai hii.

Kwa hiyo, hata Kitaifa tumekuwa na vikao nao tunawaambia msije kwenye vikao vyetu kabla ninyi wenyewe hamjakaa kama *NaCoNGO* ngazi zote mkaongea yale mnayotaka kuwasilisha Serikalini chini ya Afisa Maendeleo ya Jamii kama mwakilishi wetu huko kwenye ngazi zenu ili mkija Serikalini mje na hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuanzia kipindi kijacho cha Kamati za Bunge letu tutaanza kuwasilisha taarifa ya utekelezaji. Wamesema nini kutoka ngazi zote, kipi tufanye Kitaifa na kipi wamekwama huko. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Thomas Maganga, swali la nyongeza.

MHE. THOMAS K. MAGANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la

nyongeza. Kwanza ninamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuniteua, na mimi ninamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tamasha linaandaliwa sasa hivi Dar es Salaam na muandaaji wa tamasha hilo mienendo yake mitandaoni imekuwa haiendani na maadili ya Mtanzania. Serikali imefuatilia kujua maudhui ya tamasha hilo, kwa sababu ikipelekea hivi tunavyoongea ukitazama mitandaoni muandaaji wa tamasha hilo kwenye picha zake za mjongeo za mtandaoni ameweka mpaka matiti wakati anaandaa tamasha hilo? Nini kauli ya Serikali kwa mwandaaji wa tamasha hilo? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kunipa fursa kujibu swali zuri la Mheshimiwa Kampala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nikiri kusema kwamba uratibu wa matamasha mbalimbali una milango mingi ya kuingia na kufanyika. Sasa ninapenda kupata taarifa zaidi pengine huenda ni tamasha liko chini ya sekta ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo au ni la sekta ipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *approval* ya matamasha yote huwa inafuata miongozo ya kisekta ambako ajenda husika inakwenda kufanyika kwenye hiyo sekta. Ninamwahidi mimi ninafuatilia taarifa kutoka kwake nijue, halafu nitawasiliana na sekta husika kama hilo lipo na kwamba tamasha hilo ni tishio kwa maadili yetu humu Tanzania, kifuatacho itabidi walioli-*approve* wawajibike kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu. Ninaomba niwaletee matangazo na tunaanza na wageni walioko Bungeni.

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wako wageni watatu Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambao ni ndugu na rafiki zake kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wapo wageni 58 wa Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi, Naibu Waziri wa Afya ambao ni wanafunzi wa UKWATA kutoka Wilaya ya Kibondo, Mkoani Kigoma. *(Makofi)*

Wapo wageni 56 wa Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro ambao ni wanafunzi na walimu wa Shule ya Sekondari Daora ya Ilala, Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wapo wageni 122 wa Mheshimiwa Aeshi Khalfan Hilaly ambao ni wanafunzi na walimu wa Shule ya Awali na Msingi ya *St. Mathias* kutoka Mkoani Rukwa. *(Makofi)*

Wapo wageni 35 wa Mheshimiwa Simon Songe ambao ni wanafunzi na watumishi wa Kituo cha Maendeleo ya Mtoto na Kijana wa Kanisa la *PEFA* Nyanso kutoka Busega, Mkoani Simiyu. *(Makofi)*

Wageni wetu karibuni sana hapa Bungeni. *(Makofi)*

Ninaomba nilete matangazo. Tangazo linatoka kwa Mwenyekiti *Bunge Sports Club*, Mheshimiwa Rebeca Nsemwa. Ninaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge na watumishi wa Bunge matokeo ya mchezo wa mpira wa kikapu *(basketball)* wanawake uliochezwa leo saa 12.00 asubuhi kwenye viwanja vya *Chinangali Park*. Waheshimiwa Wabunge walishinda 28 na watumishi wa Bunge 16 na nyota wa mchezo huo alikuwa Mheshimiwa Esther Matiko. *(Makofi)*

Aidha, Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* anawakumbusha kuwa kesho Siku ya Alhamis kutakuwa na mpambano mwingine mkali wa mchezo wa kuvuta kamba kwa wanawake kati ya Waheshimiwa Wabunge na watumishi wa Bunge. Michezo yote inalenga maandalizi ya Mashindano ya Mabunge ya Jumuiya ya

Afrika Mashariki. Mnaombwa kujitokeza kwa wingi kwenye Uwanja wa Jamhuri saa 12.00 asubuhi. *(Makofi)*

Tangazo lingine linatoka kwa Katibu wa Bunge, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kuwa Klabu ya Bunge ya Michezo inaendelea na mazoezi ili kujiweka sawa kwa mashindano mbalimbali ya michezo ikiwa ni pamoja na Mashindano ya Umoja wa Mabunge ya Afrika Mashariki yanayotarajiwa kufanyika Disemba 2026. Hivyo, ninapenda kuwajulisha kuwa zoezi la usajili wa wachezaji kwa kila mchezo linaendelea katika viwanja vya michezo vya Jamhuri, Chinangali, *Roma Complex* na Kilimani.

Waheshimiwa Wabunge wanamichezo mnakumbushwa kuhudhuria na kushiriki kikamilifu katika mazoezi haya kila siku ili kukamilisha zoezi hilo muhimu la usajili wa timu. Aidha, umahiri na ushiriki wa mazoezi kikamilifu utaongeza kigezo cha kusajiliwa katika mchezo husika. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo pia kutoka kwa Katibu wa Bunge; Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 127(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge ya Mwaka 2025, leo tarehe 10 Juni, 2026 ndiyo zimekamilika siku sita za Serikali na Kamati ya Bunge kufanya majumuisho kwa kuzingatia hoja zenye maslahi kwa Taifa, zilizojitokeza wakati wa kujadili bajeti za Wizara kwa mwaka wa fedha unaoishia na makadirio ya matumizi ya Wizara hizo kwa mwaka wa fedha unaofuata.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 127(5), (6) na (8) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, mnataarifiwa kuwa siku ya kesho Alhamisi tarehe 11 Juni 2026 kuanzia saa 10.00 Alasiri, Waziri wa Fedha atasoma Bungeni Hotuba ya Bajeti ya Serikali. Siku hiyo itatanguliwa na Waziri wa Mipango na Uwekezaji kutoa maelezo kuhusu hasi ya uchumi kwa ujumla. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mnakumbushwa na kuhimizwa na inasisitizwa kesho kuhudhuria bila kukosa, ili kusikiliza maelezo ya hali ya uchumi wa nchi na bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2026. *(Makofi)*

Mwisho wa matangazo.

Baada ya haya ninaomba kuahirisha Shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

(Saa 5.29 Asubuhi Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 11 Juni, 2026 Saa Tatu Asubuhi)

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA